Kikao cha Nane – Tarehe 06 Oktoba, 2017

Kikao kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe katika kikao cha Baraza la Wawakilishi tarehe 2/10/2017 Mhe. Miraji Khamis Mussa wa Jimbo la Chumbuni aliuliza swali la nyongeza kwa Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais na Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais aliahidi kujibu kwa maandishi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 40 (4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016 sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mjumbe huyu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Miraji Mussa Khamis Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni swali lake la nyongeza alilotaka kujua ni asilimia ngapi za serikali imeshatumia katika kipindi hichi cha robo ya kwanza ya mwaka 2017/18 katika Bajeti ya Maendeleo. Mhe. Mwenyekiti jibu kama ifuatavyo:-

Kwa robo ya kwanza ya mwaka 2017/18 serikali imeshatumia jumla ya shilingi bilioni kumi na tatu nukta sita moja saba sawa na asilimia sabini na sita nukta nane ya fedha za maendeleo, sawa na asilimia kumi na moja nukta saba ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 2017/18. Naomba kuwasilisha. Ahsante.(*Makofi*)

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2016-2017.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati mezani kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2016-2017.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 67

Baraza la Manispaa kukamata Mikokoteni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu kwa dakika moja tu nitoe neno la shukurani kama utaniruhusu.

Mhe. Mwenyekiti: Unasemaje Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikiomba dakika moja tu nitoe neno la shukurani Mhe. Mwenyekiti kabla ya kuuliza swali langu

Mhe. Mwenyekiti: Uliza swali Mheshimiwa kwanza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante.

Mheshimiwa jana tulikuwa na chaguzi baadhi ya sehemu za ngazi za CCM chama kikubwa kuliko Vyama vyote Tanzania niwapongeze wale walioshinda na Chama chetu cha Mapinduzi ambacho ni chaka kikubwa kuliko vyama vyote Tanzania tuna "msemo hakuna mshindi kuna anaeongoza".

Nichukuwe fursa hii kumpongoza Mnadhimu wetu wa Chama cha Mapinduzi baada ya kutufikiria Mhe. Ali Salum Haji. Baada ya maelezo hayo naomba suala langu namba 67 lipate jawabu.

Mnamo tarehe 19/7/2017, Watendaji wa Baraza la Manispaa walikamata mikokoteni 4 na vespa 3 zilizoegeshwa katika eneo la Darajani.

Je, ni sababu gani zilizopelekea vyombo hivyo vikachukuliwa na wahusika wa vyombo hivyo ni akina nani.

Mhe. Waziri wa Nchi OR Tawala za Mikoa, Serkali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba na kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7/2014 imetoa Mamlaka kwa Serikali za Mitaa pamoja na mambo mengine kuchukuwa hatua za kuhakikisha kuwa barabara zote zilizomo katika maeneo yake ya utawala zinapitika kwa hali ya usalama. Jukumu hili linahusisha pia suala la maegesho yaani *Parkings* katika maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kusimamia Sheria hiyo pamoja na Kanuni za Serikali za Mitaa husika, Mamlaka zimekuwa zikiwachukulia hatua watumiaji wa vyombo wanaokiuka taratibu za maegesho kwa kuweka vyombo vyao katika maeneo yasiyo rasmi wakiwemo waendesha mikokoteni na vespa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake namba 67 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ haina majina ya wamiliki wa mikokoteni minne na vespa tatu ambao vyombo vyao vilichukuliwa na Watendaji wa Baraza la Manispaa mnamo tarehe 19/07/2017 ambapo ninaamini hilo lilifanyika baada ya vyombo hivyo kuegeshwa katika eneo lililopigwa marufuku Kisheria hapo katika eneo la Darajani. Ninawashauri wenye vyombo ambavyo vinafikiwa na kadhii hii kufika Ofisi za Baraza la Manispaa ili kumaliza jambo hili kwa kufuata taratibu ziliopo Kisheria. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kusikitisha ya Mhe. Waziri nanukuu tarehe 4 Juni 2014 Mawaziri jibuni maswali ya Wawakilishi kwa hoja aliyotoa Dkt Ali Mohd Shein na ya pili akatumia kauli yake "*Qul khaqum Waqul- Muruwa".* Anayozungumza Jaku Hashim Ayoub ni sawa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo hivi vina namba, mikokoteni naweza kusema kwamba bahati mbaya haina namba ukienda *ZRB* unaweza kupata namba, ukienda Bima unaweza kupata Namba haya ni majibu ya kusikitisha Mhe. Waziri. Suala nimelitaja tarehe na tukio lilipotokea. Lakini vespa zina namba hata sijui Mheshimiwa Waziri umejibu nini mtihani mkubwa. Vespa zina namba ukienda Bima utapata mmiliki, ukienda *ZRB* utapata mmiliki mikokoteni tuseme kwa bahati mbaya. Kwa hiyo, haya majibu Mhe. Mohd Aboud wewe ndie mtendaji Mkuu wa shughuli hizi katika Baraza mnatupa shida kuuliza maswala. Ni sababu gani ....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Haku Hashim Ayoub naomba uulize swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekkiti, ni sababu gani Mhe. Waziri ukashindwa kuzijua namba hizi wakati vespa zina namba, mikokoteni bahati mbaya. Lakini zoezi hili limefanyika Mhe. Waziri pahali panaruhusika ziko *parking* zimeenda kuchukuliwa usiku tu.

Mhe. Waziri wa Nchi OR Tawala za Mikoa, Serkali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nitoe masikitiko makubwa kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub pale anapouliza swali kutaka ajibu anavyotaka yeye na sio kujibiwa kisheria.

Mimi nimejibu suala hili kwa mujibu wa sheria na kanuni zilioko. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu mama vyombo hivi vilikamatwa kwenye tarehe 19/7/2017 katika eneo la Darajani pahala pasiporuhusiwa kisheria na wa miliki wa vyombo vyote kwa kutambua kwamba wamevunja sheria walifika Mahakamani kwenye Mahakama ya Manispaa na wakatozwa faini ya shilingi elfu kumi kila mmoja.

Sasa sioni hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub hapa anazungumzia nini kwa sababu watu wamevunja sheria wamekamatwa wamefikishwa Mahakamani wametozwa faini kila mmoja shilingi elfu kumi kwa kutambua hilo wao wameridhika na hilo. Sasa waliohusika wameridhika na maamuzi ambayo yamefanywa kisheria. Sasa Mheshimiwa Mwakilishi

alitaka kujua faida na utaratibu uliotumika ndilo jibu ambalo nimekuja nao Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimekuona kuhusu utaratibu nakuomba ukae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sasa mnatupa kanuni Mhe. Mwenyekiti, kanuni mnetupa tuzitumie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nakuomba ukae na tunaendelea.

Nam. 104

Matengenezo ya Mitaro ya Meli Nne Uzi na Shunda

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza**:**

Wananchi wanaoishi karibu na mtaro wa maji ya mvua wa Meli Nne kwa Shunda na mtaro wa Meli Nne Uzi, mara nyingi wakati wa mvua za masika hupata tabu na usumbufu mkubwa wa kuingiliwa na maji nyumba zao. Kwa kuwa tatizo hilo lipo kwa muda mrefu sasa,

(a) Je, Wizara kupitia Manispaa ya Magharibi "B" ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo mitaro hiyo.

(b) Kama matengenezo hayo yatafanyika, ni lini yataaza kufanyiwa kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 104 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa wananchi wanaoishi karibu na misingi ya maji ya mvua wa Meli Nne kwa Shunda na msingi wa Meli Nne Uzi mara nyingi huwa wanakabiliwa na tatizo la kuingiliwa na maji katika makaazi yao wakati wa mvua.

Mhe. Mwenyekiti, katika kulitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia Baraza la Manispaa Magharibi B tayari limeyafanyia matengenezo madaraja matatu ambayo ni Daraja la kwa Shunda, Daraja la Kijitoupele na Daraja la Uzi yaliyomo katika mitaro hiyo. Kazi hiyo imefanyika kwa mashirikiano makubwa

kutoka kwa Mhe. Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele kupitia fedha za Mifuko ya Jimbo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii ya kipekee kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele kwa kutekeleza wajibu wao wa kuondoa kero kwa Wananchi kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Naomba tuendelee kushirikiana pia katika kutoa taaluma kwa wananchi wa maeneo husika katika kuitunza misingi hiyo ili iweze kupitisha maji nyakati za mvua kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali ya Mitaa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa jibu lake zuri na lengo letu sisi ni watumishi wa wananchi wetu katika jimbo letu na kwenye matatizo yoyote yanayojitokeza kwa matatizo kwa jamii tunaruhusika sisi tulete hapa ili serikali itekeleze kuondoa kero hizi. Suala langu liko hapa.

Kwa kuwa ujenzi wetu wa madaraja yetu haya tumefanikisha kwa asilimia mia moja vizuri. Lakini bado mtaro wetu huu hasa unaotoka kwa Shunda kwenda zake mpaka Ziwa Maboga bado una kero kubwa huko mbele.

Je, Mhe. Waziri kupitia Manispaa yetu kwa kushirikiana na mfuko wa Mbunge na Mwakilishi utatuwekea utaratibu gani mzuri wa kuhakikisha kwamba tunahami eneo hilo ili kuwanusuru wananchi wetu waoneondokane kabisa na tatizo la mvua pindi zinapotokea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa wananchi jimbo la Kijitoupele suala lake kama ifuatavyo:

Kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu wa Serikali za Mitaa tunazipokea pongezi za dhati kutoka kwa Mhe. Mwakilishi.

Ni kweli kabisa Mheshimiwa mtaro huu unaungana pamoja na maji yanayoelekea kwenye Ziwa Maboga. Nataka nimuhakikishie kwamba kama tulivyoshirikiana katika ujenzi wa madaraja haya tutashirikiana vile vile katika uimarishaji wa miundo mbinu ya madaraja haya yatakayoungana na uondoshaji wa maji ya mvua yale yanayotoka Ziwa Maboga na yale ya Mwanakwerekwe. Serikali inao mpango wa kutengeneza misingi mikubwa kupitia mradi wa *ZUSP II* kwa ajili ya kurekebisha kadhia ya maji ya mvua yanayotoka katika madaraja haya Bonde la Mwanakwerekwe, Ziwa Maboga ili maji hayo kuyasafirisha na kuyaunganisha katika Bonde la Sebleni na Mtaro unaoelekea kwa Binti Amrani. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana wakati ukifika wakati wa utekelezaji wa mradi huu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza kwanza namshukuru na nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na wafanyakazi anaoshirikiana nao kwa majibu mazuri aliyotupa ambayo yanatupa uhai mkubwa katika kutatua kero hizi za mitaro yetu hapa nchini.

Mhe. Waziri katika majibu yako ulitwambia kuna mradi wa *ZUSP II* ambao unategemea kutatua kero hizi. Lakini Mhe. Mwakilishi alipoinua alionesha changamoto ya wazi wazi katika mtaro huu ambapo kuna maji yanatuwama wakati wa mvua hayaendi katika mtiririko wake.

Je, serikali imeshafanya upembuzi yakinifu katika eneo hili kujua tatizo liko wapi ili kuja kuondoa kadhi hii ambayo inawakumba watu hawa wa daraja la kwa Chunda na kama imefanya upembuzi yakinifu ni gharama gani tunategemea zitatumika ili kuondoa tatizo hili wakati huo wa utekelezaji wa mradi huo wa *ZUSP II*. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chumbuni suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli Mheshimiwa Mwakilishi alipokuwa akiuliza swala la nyongeza alionesha changamoto za wazi wazi na ndio maana nilitoa jibu la kwamba tutaendelea kushirikiana ili kuzitatua changamoto hizo. Lakini suala lake kuhusu upembuzi yakinifu serikali imefanya upembuzi yakinifu na ndio maana tukafikiria suala la kuweza kuwa na mradi mkubwa sana ambao utagharimu pesa nyingi, kama ule mradi ambao umefanyika katika Jimbo lako la Chumbuni Mhe. Miraji, Jimbo la Mpendae na Jimbo la Jang'ombe na majimbo mengine kwa kupitia *ZUSP One*. Kwa hivyo, kwa sababu mradi huu ni mkubwa, serikali ililazimika kufanya upembuzi yakinifu. Kwa hivyo, upembuzi yakinifu upo.

Kwa hivyo, suala la gharama kiasi gani. Mimi nadhani hili Mhe. Miraji Khamis uendelee kutuvumilia kwa sababu gharama zitajulikana baada tu ya kutengeneza zile *BOQ* kwa ajili ya kuwapata wakandarasi, na *still* baada ya kujua hivyo bado itabakia kuwa ni siri kwa sababu baadae itabidi tutangaze *tender*, hatuwezi kutaja *amount* ambayo itagharimu miradi hii. Ahsante sana.

Nam. 34

Uvaaji Sare Kwa Watumishi wa Umma

Mhe. Suleiman Sarhan Said - Aliuliza:-

Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa sababu asubuhi, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema mwenye kurehemu, aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote na tumtakie heri Mtume wetu Mohammad (SWA).

Pia tumtakie afya njema Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Mwenyekiti, naomba swali langu nambari 34 Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora lijibiwe.

Katika taasisi mbali mbali za Serikali kumekuwa na tatizo la watumishi wa umma kutovaa sare zinazowatambulisha na hivyo kuleta usumbufu kwa wananchi wanaofika katika taasisi hizo kwa ajili ya huduma.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.
(b) Kuna ugumu gani wa kuwaweka wafanyakazi wa Serikali kwa Wizara na Idara katika sare za nguo za Ofisini.
(c) Je, Serikali ina mpango gani na lini suala litapatiwa ufumbuzi kuondoa tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.34 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali hili naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, utaratibu wa kivazi katika sehemu ya kazi kwa Mtumishi wa Umma umeelezwa katika Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014. Kanuni ya 34(i) kwamba Mtumishi wa Umma atalazimika kuvaa kivazi kilicho safi, chenye kuhifadhi heshima yake na kinachokubalika katika Maadili na Utamaduni wa Kizanzibari wakati akiwa kazini.

(a) Mhe. Mwenyekiti, serikali inatambua kwamba wapo watumishi wasiovaa sare wawapo kazini. Pamoja na uzuri na umuhimu wa wafanyakazi kuvaa sare, lakini kutokana na bajeti serikali kwa hivi sasa haiwezi kuwapatia sare watumishi wake wote. Hata hivyo, Kanuni ya 34(2) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba ‘’Iwapo mtumishi wa umma anahitajika kuvaa sare katika sehemu ya kazi, sare hiyo itatolewa kwa gharama za serikali’’ mwisho wa kunukuu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaona umuhimu wa kuwaweka wafanyakazi wake wa wizara na idara sare, kadiri hali ya fedha itakaporuhusu. Hata hivyo, serikali haikuzuwia watumishi wenyewe binafsi au taasisi za umma kuwaruhusu watumishi wake kuvaa sare, iwapo watumishi husika wanao uwezo wa kugharamia sare hizo.

(c) Mhe. Mwenyekiti, serikali itaendelea kutekeleza matakwa ya sheria na kanuni za Utumishi wa Umma, na haitasita kutatua tatizo la wafanyakazi husika kupatiwa sare kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa serikali inafahamu umuhimu wa tatizo hili na kwa kweli linaleta usumbufu sana katika mawizara, unaweza kwenda pale ofisini ukamuuliza mtu wewe unafanyakazi hapa akakuambia na mimi nimekuwa mteja kama wewe. Sasa linakuwa na usumbufu mkubwa sana

(a) Swali linakuja hapa, kwa kuwa serikali inafahamu umuhimu wa suala hili Je, angalau kuna mchakato uliokwishaanza wa kuweka alama zile za rangi katika kila wizara, ili angalau wale watu wengine waweze kujinunulia wenyewe au kuanza kuja kwamba sare hizi zinafuata katika wizara fulani.

(b) Pamoja na kwamba serikali haina uwezo wa wafanyakazi wote kuwapatia, angalau kuna wizara moja imeanza mchakato wa kuonyesha kwamba tumeanza na wizara hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Suleiman Sarahani arudie maswali yake, kwa sababu sijamsikia vizuri.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, namuuliza Mhe. Naibu Waziri, pamoja na majibu mazuri aliyonipa lakini ninachomuambia Mhe. Naibu Waziri ni kwamba, katika mchakato ambao kwa sababu nafahamu umuhimu wa serikali.

(a) Je, serikali angalau imeanza mchakato wa kubuni rangi za kila wizara?

(b) Kuna angalau wizara angalau moja imeshaanza kuwafanyia utaratibu wa kuwapatia sare?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake Mhe. Suleiman Sarahan Said, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali mama kwamba wizara inaona umuhimu wa wafanyakazi wake kuwa na sare. Lakini hata hivyo, serikali imekuwa ikifanya jitihada za kutosha ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wake wote watapatiwa sare pale hali itakaporuhusu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjulishe tu Mhe. Suleiman Sarahani kwamba ni kweli wafanyakazi wetu wanapokuwa na sare inakuwa hata huduma zinakuwa nzuri zaidi. Lakini hata hivyo, kwa kupitia hilo tumetoa vitambulisho kwa wafanyakazi. Kwa hivyo, pale ambapo wahusika watakapopata matatizo yoyote katika kupata huduma katika mawizara yetu au maidara, basi ni vyema kuviangalia vitambulisho vya wafanyakazi hao na pale ambapo tatizo litakuwepo basi ni vyema kuwasiliana na wahusika kwa maana ya viongozi wa idara au mashirika hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo kuamka salama. Lakini pia nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake sahihi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nisaidie kidogo na hasa nimsaidie Mhe. Suleiman Sarahan kuhusu suala la sare. Mhe. Mwenyekiti, sare ni kweli ni jambo zuri sana na sote tunaliunga mkono. Mimi naelewa kwamba katika taasisi zetu nyingi hasa mashirika tayari sasa hivi wana sare zao. Ukienda benki, bandari, *ZECO* na maeneo mengine kama hayo, tayari mashirika haya yameweza kuamua kabisa kuwa na sare zao, ni jambo zuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza serikali imetoa toleo kwamba wavae vile vitambulisho vya kuonesha majina yao na dhamana zao ili wajulikane. Kwa hivyo, ni hatua ya mwanzo tutakwenda kidogo kidogo mpaka tutafika huko. Baadhi ya maeneo au hata katika maskuli walimu katika maskuli wanavaa sare, lakini tatizo lililokuwepo hawavai sare kwa skuli zote, kila skuli inaamua kuwa na sare yake. Lakini na ofisi vile vile tunahitajia kuwa na sare maalum za wafanyakazi wote kama vile matarishi na wengineo, madereva tunahitajia kuwatafutia nguo maalum ili watambulikane kwamba hawa ni wafanyakazi wa serikali. Kwa hivyo, juhudi zitafanyika ili tuone kwamba hili suala tumelichukulia hatua, ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia njema kabisa ilianzisha sare za wanafunzi katika nchi nzima, kwenye skuli za serikali na skuli za binafsi, hilo natoa pongezi kwa dhati kabisa kwamba linaendelezwa vizuri.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri walimu wetu hasa kinamama walijiwekea utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba wanakata sare katika maskuli yao na kuonesha kwamba walimu wa skuli fulani wana sare hii. Hilo ni pambo zuri na wanaeleweka kama ni walimu wamekwenda na sare moja.

Je, kwa kuwa mpango huo katika skuli zetu umebadilika sasa hivi. Kuna baadhi ya maskuli utawakuta walimu wamevaa mabaibui na wengine kama maninja wanasomesha na mabaibui yao bila kujulikana hii hali yake iko vipi.

Je, mwalimu huyu au tatizo hili Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kupitia Wizara ya Utumishi wanalielewa suala hilo. Kama wanalielewa ni hatua gani za uelekezaji ambazo watatoa juu ya kutafuta sare zinazokubalika, kuliko vazi ambalo wanalivaa wakati mwengine hatujui usafi wa mtu yule.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kusema kwamba suala hili

bila shaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali watakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kulijibu.

Nam. 122

Tozo ya 2% Kwa Wanunuzi wa Umeme

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Machano Othman Said) – Aliuliza:-

Katika kuimarisha huduma za miundombinu, serikali ilianzisha tozo la 2% kwa wateja wote wa ununuzi wa umeme hapa Zanzibar.

(a) Hivi lengo la serikali katika kuanzisha tozo hilo la 2% lilikuwa ni nini.
(b) Ni kiasi gani cha fedha kimepatikana tangu kuanza kwa tozo hiyo.
(c) Ni maeneo gani ambayo yamefaidika na fedha hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.122 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mhe. Mwenyekiti, lengo la serikali la kuanzisha tozo ya asilimia 2 ya miundombinu ni kuimarisha huduma mbali mbali za miundombinu kwa wananchi, ikiwemo miundombinu ya umeme kwa madhumuni ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.
(b) Mhe. Mwenyekiti, tokea kuanzishwa kwa tozo hiyo ya miundombinu hadi kufikia mwezi wa Juni 2017, jumla ya shilingi 2.18 bilioni zimekusanywa kupitia mauzo ya umeme.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Serikali wa Miundombinu unachangiwa na tozo kutoka katika huduma tofauti ikiwemo na huduma ya umeme. Kwa ujumla mfuko huu hutumika katika kugharamia uimarishaji wa miundombinu mbali mbali, ambapo kwa upande wa umeme mfuko huo umeweza kusaidia upelekaji wa huduma ya umeme katika kisiwa cha Fundo. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Naibu Waziri, hivi majuzi tu tulipitisha nguvu, waziri wako hapa akapitisha nguvu na nikaja na hoja ambayo iko kinyume na utaratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kikatiba. Hii inaumiza wananchi.

Kuna msemo niliupata hapa ng'ombe wa mbele hataki kwenda anapingwa ng'ombe wa nyuma. Wananchi hivi sasa wanazidi kuumia na gharama hii ya umeme na tumeona maisha yalivyokuwa magumu muda huu.

Je, ni sababu gani za msingi kutokufikiria kushusha umeme ule bei, ambapo waziri hana mamlaka ya kuandisha bei, na kaenda kinyume na Katiba ya Zanzibar na Kanuni za

Baraza la Wawakilishi. Ni lini utashushwa umeme ule gharama alizopandisha waziri, ili asije akapelekwa Mahakamani waziri wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, sababu kubwa ni gharama za uendeshaji. Lakini licha ya bei ambayo unahisi imepandishwa, napenda nikuambie au niwafahamishe Wajumbe na wananchi wote kwa jumla, bado bei yetu ya kununua umeme Zanzibar ni nafuu kuliko kule ambako tunauchukua. Nina maana kwamba wananchi ambao wanaishi Tanzania Bara bado wananunua umeme kwa bei ya juu ukilinganisha na wananchi ambao wako Zanzibar.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba tufahamu kwamba kutokana na uendeshaji wa gharama za umeme. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na niipongeze serikali chini ya uongozi mahiri wa Dk. Ali Mohammes Shein, katika kupeleka maendeleo katika vijiji mbali mbali vikiwemo hivyo vya Fundo, Shamiani na vijiji vyengine.

Swali langu ni kwamba mbali na kupeleka umeme katika visiwa hivi kwa kutumia mfuko huu wa tozo. Je, ni visiwa vingapi vingine ambavyo havijapelekewa umeme na serikali ina mpango wa kupeleka umeme katika visiwa hivyo ili kutumia mfuko huu wa tuzo na wananchi wapate huduma nzuri ya maendeleo katika nchi yao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali moja la nyongeza Mhe. Nassor Salim Ali Jaziri kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, visiwa vitatu bado hatujapeleka umeme na Wizara ya Fedha Mipango tayari sasa hivi imejipanga kwa kisiwa cha Kokota, fedha kutokana na miundombinu hii tayari ziko Wizara ya Fedha na Mipango, na sisi tayari tunajiandaa. Kwa hivyo, naomba Wajumbe wajuwe kwamba bado visiwa vitatu na kimoja kipo katika maandalizi ambacho ni Kokota.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimekuona. Kanuni ya ngapi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni ya 37 naitumia Mhe. Mwenyekiti. Waziri au mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo, atakuwa na wajibu wa

kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi. Isipokuwa kwamba swali hilo aliloulizwa waziri mmoja anaweza kujibu waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, nilipomuuliza swali Mhe. Naibu Waziri nilisema, ni sababu gani za msingi Mhe. Waziri aliyopandisha umeme ule kwa asilimia 20, ambapo sheria haimruhusu na mwenye mamlaka yale ni *ZURA*, waziri akaja akatangaza kupandisha, jawabu sijalipata.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, umesimama kwa kifungu hicho, lakini nahisi Mhe. Waziri alikujibu, labda hujaridhika na jawabu lake lakini jawabu alikupa waheshimiwa naomba tuendelee. Mhe. Suleiman Ali wa Ziwani kwa swali la mwisho la nyongeza.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, mimi naitwa Suleiman Makame Ali. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Lakini kabla ya kumuuliza Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kunukuu ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo tunaitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 154, inasema Sekta ya nishati hususan umeme ni nyenzo muhimu katika kukuza uchumi na maendeleo ya jamii. Aidha, matumizi ya nishati ya umeme hurahisisha shughuli nyingi za kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, katika jimbo langu kuna sehemu inaitwa Ngagu Mkumbuu ambako ndiko ulikopitia umeme kutoka Tanga, na kuna wakaazi si chini ya 100 kule, mpaka hadi leo hii hawana umeme.

Je, ni lini wananchi wake watafikishiwa umeme ili kuhakikisha kwamba na wao wanakabiliana na maisha katika masuala haya ya umeme na kuweza kufanya biashara zao kama inavyotakikana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali wa Ziwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza kabla sijamjibu tuna ahadi kwamba nitafika kwenye jimbo lake, basi naomba nichukuwe nafasi hii kumuambia kwamba nikifika tutafuatana na watu wetu wa umeme wa *ZECO* kusudi kuona tunafanyaje. Kwa hivyo, jawabu ni lini baada ya kufika huko ndio itajulikana, ahsante sana.

Nam. 51

Masafa Makubwa ya Skuli Kwa Wanafunzi Katika Skuli ya Kiuyu Kipangani

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Lakini kabla ya majibu, ningependa nifanye masahihisho kidogo kuna jambo limejitokeza ambalo lilikuwa sio sahihi. Pale inaposomeka masaa 6. Sio masaa 6 ni maili 6. Kwa hivyo, isijekuonekana kwenye *Hansard* kama mimi nimesema watu wanaondoka masaa 6 wanafuata skuli. Huko skuli wakifika wanakwenda kusoma masaa mangapi. Hapana, ni maili 6. Naomba nipewe jibu pamoja na marekebisho yake, ahsante swali langu naomba lijibiwe.

Kwa kuwa wakati wa ziara ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, alipotembelea skuli ya Kiuyu Kipangani mwaka 2016, wananchi walilalamika juu ya dhiki kubwa ya watoto wao wanaomaliza darasa la 6 kutembea masafa marefu kufuata skuli ya Konde ambapo ni takriban kama masaa (6) na kwa sababu ya mazingira hatarishi ya usalama ya wanafunzi wa kike yaliopo kwenye msitu wa Ngezi wanafunzi huamua kusitisha masomo hali wana kila sababu ya kuendelea na masomo yao.

(a) Je, ni lini Wizara itaanzisha darasa la Form I kwa shule ya Kiuyu Kipangani kuwawezesha watoto wa Kiuyu Kipangani, Bandari Kuu, Kiuyu Kibatini Mshashani na vijiji vya jirani kupatiwa elimu ya Sekondari katika skuli ya Kiuyu Kipangani, jambo ambalo Mheshmiwa Waziri aliahidi kulishughulikia kwa haraka.

(b) Je, ni sababu gani ya msingi inayosababisha Wizara kutoanzisha darasa la sekondari katika skuli hiyo.

(c) Je, kunahitajika walimu wangapi wa kuanzia kwa masomo yote yanayofundishwa ya sekondari ili kusaidia kuanzishwa kwa darasa hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -
Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo: -

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaifanyia kazi ahadi ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo Amali ya kuanzisha darasa la "*Form 1*" katika skuli ya Kiuyu Kipangani kwa kukamilisha taratibu na kufikia vigezo vya kuanzisha darasa la sekondari vigezo hivyo ni kama vile Idadi ya wanafunzi wa kutosha, idadi ya walimu wa kutosha , idadi ya madarasa ya kutosha na vigezo vyengine ambavyo vinatakiwa katika kukamilisha skuli ya Sekondari

Hata hivyo Wizara yangu inatarajia kuanzisha darasa hilo katika mwaka wa masomo unaoanzia Januari 2018.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza, hapa kwenye jibu Mhe. Waziri mengine hakuniambia nililonalo mie lakini yeye kaongezea si vibaya, lakini kataja vigezo kwamba iwe ishirini na walimu 10

Je, kwa kuwa kutakuwa na ongezeko hilo la walimu na mwendo ni mrefu kama nilivyosema kama masafa haya ni marefu na walimu wanatakiwa waende pale wawahi kusomesha vipindi kwa wakati muafaka. Je hayo mengine sawa, lakini je mmejipanga vipi Wizara kuwapatia makazi walimu watakaokaa pale kufundisha katika hiyo skuli ya Kipangani pindipo likianzishwa hilo darasa la *Form I* ambalo tunategemea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kabla ya kujibu niseme kwamba katika kuanzisha madarasa ya Sekondari kuna vigezo vyake na vigezo hivyo baada ya kukamilisha ndivyo Wizara inaamua kuanzisha darasa, tunazingatia sana kuhusu upatikanaji wa walimu waliopo katika maeneo ya karibu na skuli hiyo ili kutatua tatizo hili la makaazi, na pale ambapo suala hili haliwezekani kupatikana kwa walimu Wizara hutoa *bus fare* kwa walimu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine.

Mh. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini napenda nimuulize suala dogo.

Mhe. Waziri katika kijiji cha Kizimbani kuna skuli moja ambayo ipo Kizimbani Migombani na skuli hii inasomeshwa mwisho darasa la saba na wanafunzi wanaoitumia Skuli ile ni kuanzia Kizimbani, Migombani, Kizimbani Popo, Mndo mpaka wengine wanatoka Kinumoshi. Je, kuna utaratibu gani wa kuendeleza skuli ile angalau kufikia ile *Form II* kwa sababu tunaona kwamba wanafunzi wanaotoka pale darasa la sita na la saba wanakuwa ni wadogo sana, lakini wanatumia masafa makubwa pia kwenda skuli ya Langoni Mikindani au kuja Kitundu.

a) Je, kuna utaratibu gani wa kuiendeleza skuli ile ili nayo ikawa na madarasa hayo ya *Form II*

b) Kuna utaratibu gani wa kuweka eneo jengine la kuendeleza ile skuli kwa sababu eneo lililojengwa ile skuli linaonekanwa ni dogo ambapo nyuma yake kuna kiwanja cha mpira, Ila hakuonyeshi nafasi ya kuendeleza tena skuli ile. Je, endapo tayari itatakiwa kujengwa au kuendelezwa skuli hii ni kiwanja gani ambacho kitatumika kuiendeleza skuli ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Muwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza napenda kusawazisha kwamba skuli zote Zanzibar zinaishia darasa la sita na sio darasa la saba kama alivyosema kama ni skuli za msingi, lakini tuseme kwamba ili skuli iweze kufanywa Sekondari kuna vigezo vyake lazima vifikiwe, kwa hivyo wakati skuli hiyo uliyoitaja itapofikia vigezo vyake basi Wizara itai- *promote* na kuendelea Sekondari, lakini pamoja na hivyo kwa kuwa sehemu nyenyewe iliyojengwa skuli labda hakuna eneo la kufanya *extension* na skuli yenyewe basi Wizara itatafuta sehemu nyengine muafaka kwa kushirikiana na Halmashauri ili kuona tunaweza kujenga skuli.

Lakini hata hivyo ni kwamba katika plan ya baadae ya Wizara bila ya shaka kupitia Wizara ya Ardhi kutakuwa na maeneo maalum ambayo yatatengwa kwa skuli na maeneo haya yatahifadhiwa, kwa hivyo kila wakati ambapo Wizara itataka kujenga skuli maeneo hayo yatakuwepo.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala la nyongeza kwa Mhe. Waziri wa Elimu, kwanza nimpongeze sana kwa majibu yake ambayo yanaonyesha uhai na utatuzi wa kero za kielimu katika nchi yetu niipongeze sana Wizara.

Lakini Mhe. Waziri katika kero za kielimu pia zimejitokeza katika Skuli ya Mgonjoni na wakati wa Ziara ya Mhe. Rais kulitoka ahadi ya kupatiwa wahudumu wawili na mlinzi mmoja.

a) Je. Mhe. Waziri ahadi hii unaitambua.
b) Kama unaitambua ni lini Wizara yako itatekeleza ahadi hii ili kero hii ya kielimu iondoke katika skuli ya Mgonjoni.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Muwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaitambu ahadi hii na itaitekeleza na taratibu za kuitekeleza zimeshaanza kwa kuombewa ruhusa na vibali vya uajiri.

Nam. 95

Ongezeko la Viwango vya Mshahara

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imetoa maelekezo ya mishahara ya kima cha chini kwa kampuni na taasisi binafsi.

(a) Je, Serikali ina mpango wa kusimamia makampuni au taasisi binafsi kuhakikisha kwamba wanawalipa wafanyakazi wao mishahara kama ilivyoagizwa na Wizara husika.

(b) Je, kwenye kipindi cha mwaka 2015/2017 ni vijana wangapi ambao wameajiriwa kwenye sekta binafsi ambao wanatambuliwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ili kufahamu uhalisia wa mchango wa sekta binafsi katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 95 lenye vipengele (a) na (b) kabla naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa uwezo alionao kwa mujibu wa kifungu cha 97(1), cha Sheria ya Ajira, nambari 11, 2006, nilitangaza kima cha chini cha mishahara kwa sekta binafsi tarehe 30 Juni, 2017 (*legal notice* – nambari 68, 2017). Tangazo hilo limechapishwa katika gazeti rasmi la Serikali Vol. CXXVI Nam. 6660 la tarehe 21 Julai, 2017 na utekelezaji wake umeanza mwezi Julai, 2017.

Mhe. Spika, baada ya maelezo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ndio Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ina mpango wa kupitia makampuni au Taasisi binafsi kuhakikisha kwamba wanalipa wafanyakazi wao mishahara kama ilivyoagizwa. Mpango huo unafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005, Kifungu cha 17, ambapo Afisa Kazi amepewa mamlaka ya kufanya ukaguzi kazi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria za Kazi nchini. Jumla ya Taasisi 55 zinatekeleza agizo hilo kati ya Taasisi 100 zilizofanyiwa ukaguzi kazi. Taasisi 45 zimepewa notisi ya kutekeleza tangazo hilo na zinafuatiliwa kwa mujibu wa notisi walizopewa. Kazi hiyo imefanywa kwa kipindi cha miezi miwili baada ya kutoka tangazo hilo.

(b) Kwa mujibu watakwimu tulizokusanya kupitia Mtandao wa Taarifa za Soko la Ajira kwa mwaka 2015/2017, jumla ya vijana 1,549 (wanawake 570 na wanaume 976) wamepata Ajira katika sekta binafsi nchini.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wazee, Wanawake na Watoto, lakini nilikuwa na swali dogo la nyongeza ambalo nilitaka kuliuliza kwa ajili ya maslahi ya Wazanzibari hasa vijana.

a) Kwa kuwa Wizara imetoa *notice* na imekiri kwamba kuna baadhi ya makampuni hadi leo bado hawajaanza kutekeleza hilo agizo, kwa sababu *notice* ya miezi miwili imetolewa kwa hayo makampuni ambayo hayajatekelezwa. Mimi kwanza nataka nijue Je, muda gani tokea kutolewa *notice* hiyo na lini itamaliza *notice* hiyo.

b) Ni hatua gani zitakazochukuliwa na Wizara yako baada ya kumaliza ule muda wa *notice* kwa zile kampuni ambazo zitashindwa kutekeleza agizo lililotolewa ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Muda uliotolewa tangu Julai ilipaswa ianze kulipa Julai, 30 na mpaka sasa hivi Septemba imekuwa inaendelea kama tulivyokuwa tumetoa agizo, wale

wote watakaokuwa hawajaweza kutekeleza suala hilo watachukuliwa sheria na hatua kali ni pamoja na wale wakaidi kupindukia wanaweza hata kufutiwa shughuli zao.

Kwa sababu lililopo hapa Mheshimiwa ni kuangalia kwamba ni muda wa miaka saba mishahara ilikuwa haijapandishwa na waajiri walikuwepo na wakilipa vima vya chini, kwa kiwango cha chini kabisa ambayo tumegundua kabisa kwamba imekuwa ikitumia *labor force* ambayo ni nyepesi na rahisi sana katika nchi yetu na wakithubutu kutumia lugha zisizofaa kwa Wazanzibari kusema kwamba hawafanyi kazi vizuri ni wavivu, wategaji wakati walikuwa wanalipa kiwango kidogo sana. Sasa kutokana na kiwango hicho ambacho kimepasishwa cha kulipa kima cha chini laki tatu ili watu waweze kufanya kazi kwa utulivu na amani na warudishiwe heshima yao ya kuambiwa kwamba Wazanzibari hawawezi kufanya kazi inapaswa walipe kwa mujibu wa tulivyoweza kutoa.

Mhe. Ame Haji Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza suala moja dogo la nyongeza.

Ni kweli jitihada kubwa zimechukuliwa na Serikali lakini Je, Mhe. Waziri unajua kwamba taasisi nyingi hasa mahoteli wameshindwa kutekeleza agizo hili na badala yake wanaendelea kufukuza wafanyakazi kila siku, na kama hivyo ndivyo Serikali ina mpango gani kunusuru jambo hilo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuulizwa suala hili naomba nimthibitishie Mjumbe aliyeuliza kwamba mpaka hivi sasa watu ambao wanalipa kwa mujibu wa tangazo tulilopewa ni kama ifuatavyo. Ambao wengi wanatuunga mkono ni Kaskazini Unguja, idadi ya taasisi zilizokaguliwa ni ni 65 zinazolipwa ni 54 ambayo ni asilimia 83%. Kusini Unguja zilizokaguliwa ni 38 zinazolipa mpaka sasa hivi ni 28 ambayo ni asilimia 74%. Mjini Magharibi zilizokaguliwa ni 70 zinazolipa mpaka sasa hivi ni 40 ambazo ni 57%. Kaskazini Pemba zilizokaguliwa ni 14 zinazolipa mpaka sasa hivi ni 6 asilimia 43%, Kusini Pemba zilizokaguliwa ni 18 zinazolipa ni 10 ambayo ni 56%.

Jumla waliotii na wanaounga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wanaojali maslahi ya wananchi wa Zanzibar na kuwapenda na kujali wapiga kura wao ni asilimia 67%.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na mimi ningependa nimuulize suali dogo tu la nyongeza.

a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kila kitu tunapotangazwa au katika utekelezaji wa mambo kinakuwa kina changamoto nimuulize Mhe. Waziri Je, una mpango gani wa kuhakikisha kwamba kulinda maslahi ya ajira hasa kwa Wazanzibari na Watanzania wote kuanzisha utaratibu wa kima cha chini kwa sekta ya tofauti hasa sekta ya utalii, sekta ya ujenzi, sekta ya usafiri. Na kama utakuwa na mpango huo utaufanya lini.

b) Ni dhahiri kwamba katika utekelezaji wa suala zima la vibarua kutoka shilingi elfu saba mpaka elfu 25 na shilingi elfu 10 mpaka 30 kumekuwa na changamoto nyingi hasa katika sekta ya ujenzi pamoja na makampuni makubwa kwa mfano *Fumba Town* pamoja na kampuni ambayo inajenga kule ya Bakharesa, lakini pia Uwanja wa Mao hadi hivi sasa unalipa Shilingi elfu 10 kwa kibarua, ambapo uwanja huu unajengwa na marafiki zetu Serikali ya Jamhuri ya watu wa China kwa ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Je, Mhe. Waziri ni sheria ipi utaichukua ili kuhakikisha kwamba Wazanzibari wote wanafaidika na hili agizo linatekelezwa kwa upande mmoja wote.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Muwakilishi naomba kumjibu Swali lake la nyongeza lenye vifungu a na b kama ifuatavyo.

Mpaka sasa hivi ni kanuni zinazofuata ambazo zimeshaandaliwa na tayari zimepelekwa kwa Mwanasheria kusubiri kutaka kutiwa saini na ziweze kutangazwa upya, viwango vyote anavyouliza vitapatikana katika Kanuni hiyo ambayo vikao vyote vinavyohusika ikiwa ni bodi ya mishahara imeshaa na imekubaliana.

Suala la wale ambao wanasema wanalipa kiwango kikubwa cha 15, na kufikia 25 na 30 nataka kumkumbusha tu muhusika aliyeuliza kama yeye ni mmoja wapo anayawakilisha kundi la wananchi ambao wanafanya kazi za muda ambao wanahitaji kuishi ipasavyo, hawaajiriwi kila siku hawa wanaajiriwa kwa muda mchache na kwa muda ambao sio wa kila siku.

Kwa hivyo kiwango kilichokubaliwa na bodi ya mishahara pamoja na wajumbe waajiri na wengine ni kwamba kiwango hicho kilikubaliwa na sio kwa upande wa Serikali peke yake, ni vikao ambavyo vimekuwa vikifanyika na kukubaliwa kuanza kulipa kiwango hicho. Suala zima la kusema ajira zitakuwaje ni kwamba ajira zinaendelea kutafutwa na watu wanaendelea kufanya na tutaendelea kufuatilia kwamba watu hawajalipa.

Suala la Mao ni kwamba mkataba waliokuwa wameleta hawa ndugu zetu wa China uliletwa kabla hatujatangaza ajira hii, sasa suala hili ni suala la kuliangalia na kulitafakari na kuona litaweza kutekelezwa jinsi gani, ahsante.

Nam. 72

Upungufu wa Madaktari wa Mifugo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Zipo taarifa kuwa Zanzibar inakabiliwa na upungufu wa madaktari wa mifugo ambao wamekuwa wachache.

Je, hatua gani zimechukuliwa kukabiliana na upungufu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wa Jimbo la Paje swali lake Nam. 72 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kukubaliana na Mhe. Mjumbe wa Baraza lako Tukufu la Wawakilishi kwamba Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inakabiliana na upungufu wa madaktari wa mifugo ambao wamekuwa wachache, katika kukabiliana na upungufu huo Wizara imechukua hatua mbali mbali za kukabiliana na tatizo hilo kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kutambuwa kuwepo na upungufu wa madaktari wa mifugo, Wizara tayari imetoa mafunzo ya huduma za msingi ya matibabu ya mifugo kwa vijana yaani *(Community Animal Health Workers)* ambao vijana hao ni 204. Vijana hao wametoka katika ngazi ya shehia na wanaendelea kusaidia kutoa taaluma na huduma za mwanzo za matibabu ya mifugo kwa Unguja na Pemba.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo, na Uvuvi imekuwa na mashirikiano ya hali ya juu na Jamhuri ya Watu wa China. Aidha, katika kutatua uhaba wa madaktari wa mifugo hapa Zanzibar, kwa miaka mitatu mfululizo Wizara imepeleka jumla ya vijana kumi na tano (15) kwa ajili ya udaktari wa

Mifugo nchini China. Vile vile, kwa mwaka 2017/2018, Wizara tayari imekamilisha utaratibu wa usaili wa vijana 16 ambao watakwenda nchini China kwa ajili ya mafunzo ya udaktari wa mifugo. Hatua hizo ni jitihada za Wizara ya Kilimo kupitia miongozo thabiti ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, katika kuhakikisha kwamba tunaondoa kabisa tatizo la uhaba wa madaktari wa mifugo. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa kukiri tuna upungufu wa madaktari, hongera sana Mhe. Naibu Waziri.

Lakini baada ya hapo naomba nimuulize swali moja lenye vifungu (a) na (b):

(a) Mahitaji ya wataalamu wa madaktari wa mifugo hapa Zanzibar tunahitaji wangapi na tuliokuwa nao wangapi mpaka muda huu.

(b) Kwa nini tija ya wafugaji wa ndani hivi sasa Zanzibar haionekani, samaki kutoka nje, kuku kutoka nje na maziwa yanatoka nje na baadae yanakuja hapa na kuvurugwa na tukatia kwenye mifuko na yakauzwa. Je, kama wizara unayoisimamia imechukuwa hatua gani kuwawezesha wafugaji, kufuga ng'ombe wa kisasa na ng'ombe wa maziwa baadae tusiagize maziwa kutoka nje na yakavurugwa na baadae yakapata kuuzwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, swali lake kama ifuatavyo:

(a) Tunamahitaji ya wataalamu wengi, na tunajitahidi sasa hivi kusomesha Chuo chetu Kizimbani kinasomesha ngazi ya *certificate* na *diploma* na wataalamu hawa tukishamaliza moja kwa moja tunawapa ajira.

Mhe: Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu…

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti kuhusu swali lake (b) ningeomba alirudie kwa sababu nimekuja kusikia mwishoni mwanzoni katika maelezo yake sijayapata vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba urudie swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti hata hilo la mwanzo hakulijibu vizuri nilivyomuuliza, alinambia wengi hata kuanzia mbili wanaweza kuwa wengi, tatu zinakuwa nyingi, nne zinazokuwa nyingi ilikuwa anitajie idadi kama hana anijibu kwa maandishi.

Swali la pili, kwa nini tija ya wafugaji wa ndani hivi haionekani samaki tunaagiza kutoka nje, kuku kutoka nje, maziwa kutoka nje baadae yanakuja na kuvurugwa na kuuzwa. Wizara yako unayosimamia nimechukua hatua gani ili kuwawezesha wafugaji kuwasaidia baadae tusiagizie maziwa kutoka nje na kuvuruga na kuuza.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, swali lake kama ifuatavyo:

(a) Kama alivyotaka nitakuletea kwa maandishi ili uwe na uhakika zaidi wa nambari ya hawa wataalamu na.

(b) Mhe. Mwakilishi akumbuke kwamba hapa kuna biashara huria, wafugaji wetu wanazalisha maziwa, ng'ombe na kila kitu lakini vile vile havitotutosheleza kwa Wazanzibari kama hatujaagiza kutoka nje ya nchi. *(Makofi).*

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuniona na kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nimpongeze Dada yangu Lulu kwa majibu yake mazuri ambayo ametupatia katika Wizara hii, lakini vile vile naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, umekiri kwamba katika wizara yako kuna upungufu wa wafanyakazi hususan hawa madaktari wa mifugo, sasa je ni mara ngapi katika mwaka au mwezi mumefanya *survey* ya kuifatilia mifugo na kuweza kuitibu kwa kupunguza maradhi ambayo yanaweza kuripuka kwa mfano kama kichaa cha mbwa na mengineyo naomba jibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar swali lake kama ifuatavyo:

Kawaida tunafanya kila baada ya miezi mitatu kupitia maafisa wetu wa wilaya vile vile, mtu yeyote ambaye ana mnyama wake labda anaumwa anafika pale Maruhubi kwa ajili ya kupata matibabu na nikuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kichaa cha mbwa kimeondoka kabisa kwa hapa Zanzibar nashukuru.

Nam. 98

Zao la Karafuu

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Zao la Karafuu Nchini ni uti wa Mgongo wa Uchumi na wananchi wetu wanaolima na kuendeleza zao hilo kadri wanavyoweza.

Kwa kuwa zao la karafuu ni zao pekee nchini tunalolitegemea, Je, Wizara yako inawasaidia vipi wananchi juu ya taaluma ya zao hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali, Mwakilishi wa Kijitoupele, swali lake kama ifuatavyo:-

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaelewa umuhimu wa zao la karafuu nchini kuwa ni uti wa mgongo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi inachukua juhudi za kuwapatia wakulima wetu taaluma katika usimamizi na uendelezaji wa zao hili.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa juhudi zinazochukuliwa na Wizara yangu ni kuwapatia elimu ya uoteshaji miche ya mikarafuu katika vitalu binafsi, kwa mwaka wa 2016/2017 jumla ya wakulima wa vitalu (75) wamepatiwa elimu ya uoteshaji bora wa miche ya mikarafuu. Unguja wakulima 9 na Pemba wakulima 66.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Shirika la *ZSTC* inawahamasisha wakulima wa karafuu kwa njia ya semina katika kila Wilaya za Unguja na Pemba. Jumla ya wakulima 445 walihamasishwa katika kilimo cha mikarafuu kwa upande wa Unguja 89 na wakulima 356 katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo pia inashirikiana na Shirika na *ZSTC* kuwapatia motisha wakulima bora wa zao la karafuu kwa kila Wilaya inayolima karafuu. Kwa mwaka 2016/2017 wakulima bora 18 walipewa zawadi ya fedha taslimu. Unguja wakulima 10 walipewa fedha, Shs.1,500,000 kwa mshindi wa kwanza na Shs. 1,000,000/- kwa mshindi wa pili, na kwa Pemba wakulima 8 walipewa zawadi hizo za fedha. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa taarifa yake au kwa swali langu zuri alilolijibu lakini pia pamoja na juhudi hiyo nzuri ya wizara kuhakikisha kwamba zao la karafuu ni uti wa mgongo katika nchi yetu. Je, vipi karibuni kumetokea matatizo ya kuungua mikarafuu mara kwa mara na taaluma ni jambo la mwaka kunusuru mikarafuu hiyo, Wizara imechukua hatua gani ya kuelimisha wakulima juu ya athari hii ambayo inajitokeza mara kwa mara. Na katika uchunguzi wao wamegundua kuna kitu gani hasa kinachosababisha hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, ningependa Mhe. Ali Suleiman Ali, swali arejee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Suleiman Ali naomba urejee swali.
Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri naipongeza wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya juu ya kuwaelimisha wananchi katika upandaji au mbegu mbali mbali kuotesha mikafuu kwa wingi, lakini pamoja na juhudi hizo ambao wanatoa taaluma mbali mbali hivi sasa kumetokea uharibifu au kuingia moto mara kwa mara katika mikarafuu mbali mbali sehemu ya Pemba, Wizara imechukua hatua gani ya kuelimisha wananchi juu ya athari hiyo.

Na pili, katika utafiti wao wamegundua kuna kitu gani, chanzo cha mikasa hiyo inayotokea mara kwa mara.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali, swali lake kama ifuatavyo:

Wizara bado inaendelea na juhudi za kuwapa taaluma wakulima hao katika kutoa juhudi hizo, wizara mara ya mwisho ilitoa vifaa vya ugawaji kwa wakulima binafsi na wakulima wa kawaida watu 170 walifaidika kupitia vifaa hivyo, vile vile, majanga ambayo unayasema yanayotokea kwenye mikarafuu tunachukua juhudi zaidi na kuzidisha ulinzi katika mashamba haya. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu, linalotokana na hujuma hizo za mikarafuu kama alivyouliza Mhe. Ali Suleiman Ali, lakini kumekuwa na tatizo Mhe. Naibu Waziri, la kuhujumu mikarafuu michanga inayozaa ndani ya miaka 5, 6 na kwenda mbele mpaka karibu ya miaka 10, wezi wanaikata wanakwenda kuchumia mbele hawachumi pale pale. Je, wizara yako inayo taarifa ya kuwa kuna hujumu wa mikarafuu kwa tokea kama hilo, na kama inayo hatua gani inachukua ili kudhibiti wimbi hili la uharibifu wa mikarafuu lisiendelee kutokea ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Wizara yangu inapopata taarifa na ikampata mtu huyo muhujumu wa mikarafuu kumchukulia hatua za kisheria zinazofaa. Lakini vile vile Mheshimiwa Mwakilishi nikiombe kwamba kazi hii ni kazi yetu sote, kwa hivyo unapowapata watu hawa basi usisite kuwafikisha katika vyombo vya sheria au katika Wizara yetu Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilitusaidiane katika kuitunza mikarafuu hii. Ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kwa majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo naomba kuongezea suala la nyongeza kuhusu zima la hujuma katika zao la karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wapo watu kwa makusudi hufanya hujuma, ima kwa kukata mikarafuu michanga, ima kwa kufanya wizi, ima kwa kuharibu vitalu vya mikarafuu na taarifa hizi zimepatikana katika sehemu mbali mbali. Ningependa nitowe wito kwa wananchi kwanza kuacha mara moja tabia hiyo, lakini tayari tumeliagiza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi kwa kina na wale wote watakaobainika kufanya shughuli za hujuma basi hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

Kwa hivyo niwaombe wananchi wawakataze watoto wao ama wapenzi wao katika kufanya jambo hilo, maana baada ya uchunguzi wa kina hatua za kisheria zitachukuliwa na hatutomuhurumia yeyote zaidi ya mkondo wa sheria kuchukua nafasi yake, kwa hivyo napenda sote tushirikiane kupambana na jambo hili ambalo lina athari kubwa katika uchumi wa taifa letu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, Mhe. Hidaya Ali Makame kwa swali la mwisho la nyongeza.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kuniona tena kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri kwanza nimpongeze sana kwa majibu yako mazuri sana ambayo yamenipa moyo lakini ningependa nikuulize swali. Mhe. Waziri kuna kina mama sasa hivi wameamua kujitoa kwenye janga la umasikini na kuweka vikundi vya ujasiri amali ili kuweza kuimarisha maisha yao pamoja na familia zao. Kina mama hao wameweka vikundi vya *SACCOS* ambavyo vikundi hivi vinajihusisha na mambo ya uatikaji wa miche hii ya mikarafuu.

(a) Je, kuna taratibu gani za Wizara kuweza kuwasomesha kinamama hawa ambao wameamua kujitolea. Kina mama hawa wako katika mikoa tofauti ikiwemo Mkoa wa Kaskazini Unguja, Donge, Mkwajuni na kwengineko.

(b) Kuna utaratibu gani wa Wizara kuweza kuwatafutia soko kinamama hawa ambao wameamua kujitoa na kuweka miche hii ili kuweza kunufaika na wao na kuendeleza sekta hii ya kilimo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Utaratibu wa kuwasomesha upo, kila leo wanasomesha wataalamu wetu na kama wanahitaji basi waje ofisi husika Idara ya Misitu, kwa barua waombe na wajiorodheshe wako wapi ili waweze kufuatwa kupewa taaluma hiyo.

(b) Kuhusiana na soko la mikarafuu Mhe. Mjumbe hapa sisi mikarafuu kwa wizara yetu tunatoa bure, lakini vitalu binafsi wanafanya biashara sana kwa hiyo hapa labda niseme wao wenyewe pia wafanye jitihada ya kutafuta soko hilo, kwa sababu sisi kama sisi tunatoa bure ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 132

Ukarabati wa Jengo la Mapinduzi Mpya Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:

Tunaipongeza Serikali na Wizara kwa juhudi zinazochukuliwa katika maandalizi ya kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa Hospitali ya Rufaa. Lakini katikati ya majengo ya kutibu ubongo na mishipa ya fahamu na jengo jipya la mapokezi, watoto, huduma za dharura na wagonjwa wa nje, kuna jengo chakavu na bovu linaloitwa Mapinduzi Mpya ambalo linaharibu mandhari yote ya eneo hilo.

(a) Lini Wizara katika mipango yake italifanyia ukarabati unaostahiki jengo hilo linalotumika kuhudumia Viongozi wa nchi wanapougua ili lionekane kweli ni Mapinduzi Mpya na kustahili kulaza Viongozi wa nchi.

(b) Kwa vile Wazanzibari tunapotaja Mapinduzi tuna maanisha utukufu kwa kile kinachonasibishwa na jina hilo, hivi Wizara haioni shida kuwalaza viongozi wetu katika jengo chakavu kama lile.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Mwanaishi Kassim Mussa, Mwakilishi wa Viti Maalum swali lake Nam. 132 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba jengo la Wodi ya Mapinduzi Mpya Mnazi Mmoja limechakaa na miundo mbinu yake imeanza kuharibika, matengenezo ya jengo hilo yamo katika mradi mkubwa wa ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, utakaogharamiwa kwa mashirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, *BADEA*, Mfuko wa Kuwait na Mfuko wa Saudi Arabia. Hata hivyo matengenezo madogo madogo ya mara kwa mara, hufanyika katika jengo hilo ili kuwezesha jengo kuweza kutumika kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuombe Mhe. Mwanaidi Kassim pamoja na Baraza lako Tukufu kwamba muondoshe wasi wasi kuhusu tatizo la uchakavu wa jengo hilo hasa kwa vile limo katika mradi wa ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Mnazi Mmoja utakaoanza hivi karibuni.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:

Kwa kuwa mradi wa ukarabati wa Hospitali utagharamiwa na wafadhili. Je, Serikali imefikia hatua gani ya makubaliano na wahisani katika ujenzi huo na unata...

NA. 5

NA. 5

NA. 6

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: (Anaendelea) ziara mbali mbali katika taasisi zetu zinazotoa elimu, tunakutana na kamati kujadili changamoto mbali mbali na pia kamati inatupatia ushauri katika kukamilisha malengo ya sekta hii. Ushauri tunaoupata tunaufanyia kazi, ili kuhakikisha kwamba changamoto hizi zinapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa ushauri tuliopatiwa hapa na kamati tunauwasilisha hapa katika Baraza lako tukufu ili wajumbe wako waweze kuelewa ufanisi wake na pia tushauri zaidi kwa lengo la kuimarisha ubora wa elimu nchini.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imepokea mapendekezo 27 kutoka katika Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi. Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba niwasilishe utekelezaji wa ushauri wa Kamati ya Ustawi wa Jamii katika maendeleo ya Sekta ya Elimu kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, pendekezo la 1.

Huduma za lazima na miundombinu ziimarishwe katika skuli za maandalizi na msingi. Upatikanaji wa huduma za lazima kama vile maji, vyoo na usalama wa skuli uhakikishwe kwa kushirikiana na mamlaka zinazotoa huduma hizo pamoja na upatikanaji wa fedha za bajeti.

Utekelezaji wa Pendekezo hili

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za lazima na miundombinu ya maji na vyoo katika skuli za Maandalizi na Msingi, Kwa mwaka 2016/17 Wizara kwa kushirikiana na wafadhili wakiwemo *(UNICEF, Milele Zanzibar Foundation, ZAWA, ADB, SOS na UMATI)* walijenga jumla ya vyoo vipya 210 vikiwemo 38 vya watoto wenye mahitaji maalumu. Aidha, vyoo 270 vilifanyiwa ukarabati, kati ya hivyo; vyoo 236 kwa Unguja na 34 kwa Pemba. Skuli zilizofaidika ni Mkunazini, Kisiwandui, Kajificheni, Hurumzi, Kiponda, Benbella, Hailesalasie, Makadara, Nyerere, Mwembemakumbi, Magogoni, Lumumba, Mwembeladu, Maungani, Kiembesamaki, Migombani, Jango'mbe msingi na sekondari, Kidongochekundu msingi na sekondari, Kisauni, Rahaleo, Muungano, Kisiwapanza, Mwambe, Michenzani na Kojani.

Katika mwaka 2017/18 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imepanga kuimarisha mazingira ya skuli kwa ujenzi wa vyoo, miundo mbinu ya maji na usalama wa skuli kwa kuwahamasisha wahisani na wananchi katika ujenzi wa uzio kwa maeneo yenye hali duni ya usalama.

Pendekezo la 2
Majengo ya skuli yafanyiwe ukarabati pamoja na kuwekwa uzio kwa maeneo yenye hali duni ya usalama, mfano skuli ya Maandalizi Madungu.

Utekelezaji
Wizara hufanya ukarabati wa majengo ya skuli mara kwa mara kutegemea bajeti na mahitaji ya skuli zinazotaka kufanyiwa ukarabati. Kwa upande wa skuli ya Maandalizi Madungu tayari wananchi walianza ujenzi wa uzio na kuziba njia ili watu na wanyama wasipite katika eneo la skuli, hata hivyo ukuta wa uzio huo umeanguka kutokana na mvua kubwa zilizonyesha Mei/Juni 2016/17 na kusababisha ardhi kupasuka. Wizara imeanza juhudi za kufanya ukarabati wa eneo hilo liloathirika kwa kuanza kujaza kifusi. Kuhakisha kuwa skuli zinakuwa katika hali ya usalama. Aidha, katika mwaka 2017/18, Wizara imepanga kuzifanyia ukarabati skuli za Haileselasie, Lumumba, na Benbella

Pendekezo la 3
Utafiti ufanyike kujua njia za kudhibiti utoro wa wanafunzi hasa katika skuli za ukanda wa pwani zenye shughuli nyingi za uvuvi na utalii, pamoja na kudhibiti wingi wa wanafunzi madarasani kwa kujenga madarasa mapya na kuajiri walimu wa msingi wa kutosha.

Utekelezaji
Wizara kwa kushirikiana na UNICEF tayari inafanya utafiti huo kwa kiwango cha ukusanyaji data kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba na wataalamu wapo katika hatua ya uandishi wa ripoti. Aidha Wizara kwa kushirikiana na Serikali, wananchi na wafadhili wanaendelea na ujenzi wa skuli mpya na madarasa ili kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani, Jumla ya madarasa 61(09 ya maandalizi na 52 yamsingi) yamejengwa Unguja na Pemba kwa mwaka 2016/17.

Madarasa hayo yamejengwa katika skuli za Binguni maandalizi madarasa (3) na vyumba (2) vya Ofisi, Skuli ya Chutama maandalizi madarasa (3) na ofisi (1), Skuli ya Jambangome madarasa (3) skuli ya Kiboje (8), Dunga (2), Bandamaji (4), madarasa (6) skuli ya Msuka, (4) Birikau, (6) Mkanyageni,Mgogoni madarasa (4) na Ofisi (1), Skuli ya Chokocho madarasa (4) na maabara, Magogoni madarasa (2) na ukumbi (1), Skuli ya Kihinani madarasa (4) na Ofisi (2), Skuli Ghana madarasa (3), Skuli ya Bwereu Msingi madarasa (4) na ukumbi (1).

Katika kudhibiti wingi wa wanafunzi madarasani Wizara kwa mwaka 2017/18 ina mpango wa kukamilisha madarasa 200 yalioanzishwa na wananchi na kujenga jumla ya madarasa mapya 48 katika skuli sita, 4 za Unguja na 2 za Pemba.

Pendekezo la 4 amablo lina vipengele kutoka a mpaka f

a. Mfumo wa elimu ya maandalizi na msingi upitiwe na kuimarishwa zaidi kwa kuhakikisha wanafunzi wanaotoka maandalizi kwenda msingi wanauwezo wa kusoma, kuandika pamoja na kuhesabu vizuri na wanafunzi wanaotoka msingi kwenda sekondari wanakuwa na uwezo zaidi wa ufahamu.

Vile vile madarasa ya maandalizi na msingi yasiwe na idadi kubwa ya wanafunzi kupitiliza ili walimu wawe na uwezo wa kumudu kufundisha kwa ufanisi. Walimu wa maandalizi na msingi wapatiwe mafunzo na nyenzo za kusomeshea kwa mujibu wa mahitaji ya maandalizi na msingi, wapatiwe vikalio na vifaa vya kujifunzia na kufundishia ili waweze kutumia gharama na ujuzi wakiwa bado wadogo

Utekelezaji wa pendekezo hili

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imo katika hatua za mwisho za matayarisho ya kufanya mapitio na marekebisho ya matamko yote ya Sera ya Elimu likiwemo tamko kuhusu mfumo wa elimu wa Maandalizi na Msingi ili iendane sambamba na malengo yaliowekwa kitaifa na Kimataifa yaani (MKUZA III na MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU **(SDG4)**

Aidha Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na shirika la kimarekani katika Mradi wa TUSOME PAMOJA inalengo la kuimarisha uwezo wa wanafunzi wa skuli za msingi katika kusoma, kuandika, na kuhesabu. Aidha, katika kuhakikisha kuwa walimu wa maandalizi na msingi wanapatiwa mafunzo na nyenzo za kutosha za kujifunzia na kufundishia, kwa mwaka 2017/18, Wizara imepanga kuwapatia mafunzo walimu wa maandalizi na msingi pamoja na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika skuli za maandalizi, skuli za msingi na katika vituo vituo vya TUTU kwa Unguja na Pemba.

Hadi kufika mwezi wa Julai 2017, jumla ya madawati 6,326, viti 3,512 na meza 2,892 vimeweza kupatikana. Jumla ya wanafunzi 25,382 wameweza kupata vikalio na kupunguza Idadi ya wanafunzi wasio na vikalio.

Kwa mwaka 2017/18 Wizara inahitaji jumla ya madawati 41,122, viti 42,204 na meza 42,824 katika skuli za Unguja na Pemba.

Katika kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani Wizara ina mpango wa kukamilisha madarasa 200 ya maandalizi yaliyoanzishwa na wananchi, kujenga madarasa mapya (48) katika skuli (6), (4) Unguja na (2) Pemba. Aidha Wizara ina mpango wa kujenga skuli mbili za maandalizi (Mlilile na Mbuyu maji), mbili za msingi (Fuoni Pangawe na Kwarara), skuli tisa za ghorofa za sekondari pamoja na kuzipatia samani zitakazojengwa kwa ufadhili wa *OPEC*. Skuli hizi zitajengwa katika maeneo ya Bububu, Mwembeshauri, Kinuni, Fuoni, Chumbuni, Ndugu kitu Chakechake, Micheweni, Kizimbani na Mwambe na skuli mbili zitajengwa kwa udhamini wa Benki ya Dunia katika maeneo ya Mwanakwerekwe na Wingwi.

b. Mashirikiano baina ya wazee, walimu pamoja na wanafunzi ni jambo la lazima kuanzia mandalizi, msingi na hata sekondari kwa kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi akiwa nyumbani, skuli na maeneo mengine ya kujifunza kama vile maktaba.

Utekelezaji

Ili kuimarisha mashirikiano ya walimu na wazazi katika kumsaidia mtoto kujifunza Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Mradi wa TUSOME PAMOJA umeanzisha kamati maalumu za ushirikiano wa Wazazi na Walimu

(UWAWA) katika skuli zote za msingi ili kuhamasisha na kushirikisha wazazi kufuatilia, kusimamia na kuchangia maendeleo ya watoto wao, pamoja na kutoa maoni inapohitajika.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na *"Madrasa Early Childhood Program"* inaendelea kuziimarisha na kuzijengea uwezo kamati za skuli ambazo zipo kisheria katika skuli zote ili kusaidia kuimarisha ushirikiano na mahusiano baina ya skuli na jamii

Wizara inahakikisha kamati hizo zinafanyakazi kwa karibu zaidi na skuli zetu ili kuweza kufikia lengo lillilokusudiwa.

c. Serikali kupitia Wizara ya Elimu ihakikishe walimu wa kutosha wanapatikana wakiwa na sifa, uwezo wa kufundisha pamoja na maadili, walimu wa masomo ya sayansi wa kutosha waajiriwe, maslahi mazuri ya kufanya kazi kwa walimu yaimarishwe

Utekelezaji
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kipindi cha Januari – Septemba 2017 imekamilisha ajira kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini, Walimu wa Sayansi 246 Unguja na Pemba kwa kiwango cha shahada na stashahada na Sanaa 67 kwa kiwango cha Stashahada Unguja na Pemba.

Aidha Wizara katika kuhakikisha maadili ya walimu yanadumishwa imefanya mafunzo juu ya sheria ya Elimu Nam 6 ya 1982 pamoja na sheria ya Utumishi wa Umma Nam 2 ya mwaka 2011 katika vituo vyake vya Ualimu kwa Mikoa ya Unguja na Pemba na kuondosha kufanya kazi kwa mazowea.

Katika kuwajengea uwezo walimu, Wizara kwa kushirikiana na mradi wa Tusome Pamoja imeanza kutoa mafunzo kuanzia mwezi wa Januari 2017 kwa Walimu, ambayo yanawawezesha wanafunzi kusoma kwa haraka kwa darasa la I na II.

Jumla ya Walimu wa Skuli 283 Unguja na Pemba wamenufaika na mafunzo hayo. Pia Wizara imepata mfadhili *"Dubai cares"* kwa kushirikiana na *"Madrasa Early Childhood Program"* katika mradi wa "watoto kwanza" unaosimamia utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu wa maandalizi jumla ya walimu 900 katika Wilaya 11 za Zanzibar wamepatiwa mafunzo hayo kwa lengo la kupunguza walimu wasiokuwa na sifa katika ngazi ya maandalizi na kuongeza ubora wa Elimu. Katika mwaka 2017/18 Wizara imepanga kuajiri walimu 929 wenye sifa na uwezo wa kusomesha kati ya hao 200 kwa Unguja 729 Pemba.

d. Vitabu na vifaa vya maabara vipatikane kwa wakati badala ya wanafunzi kupatiwa vifaa hivyo miezi michache kabla ya kufanya mitihani.

Utekelezaji
Wizara imegawa vitabu vya sayansi 192, vitabu vya sanaa 335, na vitabu vya somo la biashara 6 kwa skuli zenye kidato cha tano na sita.

Kwa kuwa skuli za Sekondari zimeruhusiwa kukusanya michango ya wazazi hadi sasa, pesa hizo hutumika katika kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya mazoezi ya vitendo. Wizara inazipatia skuli vifaa vya maabara kwa ajili ya mitihani ya Taifa. Katika robo hii ya Julai–Septemba jumla yaTzs 139 milioni zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa vya mitihani ya kidato cha nne ambayo inatarajiwa kuwa karibuni.

Idara inaendelea na ununuzi wa vifaa na vitabu vya ziada kwa skuli za kidato cha tano na sita kwa masomo ya sayansi na Sanaa.

e. Serikali irejeshe huduma dakhalia kama ilivyokuwa zamani, ili kuweka mazingira tulivu ya wanafunzi kujisomea.

Mhe. Mwenyekiti, pendekezo hili tutalizungumza katika utekelezaji wake katika agizo nambari 10 ambalo linafuata mbele yake.

f. Skuli za Msingi na Sekondari zipatiwe maktaba na vitabu, ili kutanua wigo wa kujiongezea maarifa kwa walimu pamoja na wanafunzi. Aidha, Serikali ifanye mpango wa kuanzisha mradi wa kujenga maktaba katika kila Mkoa na Wilaya.

Utekelezaji
Lengo kuu la Shirika la Huduma za Maktaba ni kuhakikisha jamii ya Zanzibar inapata huduma za Maktaba vikiwemo vitabu, machapisho na huduma za mtandao katika maeneo yote ya Mjini naVijijini

Shirika katika kufikia azma hiyo linaendelea kutafuta njia mbalimbali mbadala za kuziwezesha Skuli za Msingi na Sekondari kuwa na Maktaba za kisasa na vitabu.

Shirika limeanza kutekeleza mpango wa kuanzisha Maktaba za Mkoa, Wilaya na jamii. Hatua za mazungumzo na wakuu wa Mikoa, Wilaya na maeneo ya Shehia ili kupata viwanja vya kujenga Maktaba zimeanza.

Shirika kwa kushirikiana na *"Book Aid International"* linaangalia namna bora zaidi ya kuzihuisha Maktaba za skuli kwa kuzifanyia ukarabati, kupeleka vitabu vya kiada na ziada, pamoja na machapisho. Katika kutekeleza mpango huo *BAI* kwa maana *Book Aid International* imesaidia kuanzisha Mradi wa Maktaba katika Masanduku kwa skuli za msingi 30 Unguja na 20 Pemba. Pia Shirika limeboresha Mazingira ya Maktaba za Watoto za Maktaba Kuu Unguja na Pemba kwa lengo la kuwajengea hamu ya kupenda kutumia Huduma za Maktaba tokea wakiwa wadogo.

Pendekezo la 5
Miundombinu na huduma za lazima katika skuli ifanyiwe ukarabati kwa upande wa majengo, kuzipatia huduma za maji, umeme na usalama katika maeneo ya skuli. Aidha Serikali ifanye mpango wa kuhakikisha usalama kwa majengo ya skuli yaliyochakaa hasa Mji Mkongwe.

Utekelezaji

Wizara kwa kushikiana na wananchi pamoja na wafadhili inaendelea kufikisha huduma za lazima katika skuli. Kwa mwaka 2016/17 Wizara kwa kushirikiana na wafadhili imekamilisha ukarabati wa skuli mbalimbali zikiwemo, Kiembesamaki msingi, Fuoni, Pale, Kinyasini, Makoba na Tumbe msingi. Wizara hufanya ukarabati wa skuli za Mjim kongwe kulingana na masharti yaliyowekwa na Mamlaka ya Uhifadhi ya Mji mkongwe. Kwa sasa Wizara imepanga kuifanyia ukarabati skuli ya Hurumzi.

Pendekezo la 6
Skuli za sekondari za Ufundi ziimarishwe kwa kupatiwa vifaa, mazingira ya kusoma na kusomesha, fani za masomo ziongezwe kwa mujibu wa mahitaji ya hivi sasa ya soko la ajira, walimu wa skuli za ufundi wapatiwe motishaili waendelee kubakia kwa kuwa wengi wao wanakimbia kwa sababu mbali mbali ikiwemo maslahi duni.

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti, moja katika kipaumbele cha Wizara yangu ni kuimarisha Skuli za Ufundi Unguja na Pemba, hii ni kwenda sambamba na kauli za Viongozi wetu ya uchumi wa viwanda. Kwa mwaka wa fedha 2017/18 Skuli ya ufundi ya Kengeja na Mikunguni zimetengewa jumla yaTzs 25,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa.

Pia skuli hizo zimepatamsaada wa vifaa kutoka Bodi ya Wakandarasi Zanzibar, vikiwemo *"computer 04, rotta 02, bench grader 01, hand grader, 01, electrical board 02, drawing board 36, patasi seti 14, na grinding machine" 01*.

Juhudi za kuimarisha mazingira ya kufundishia katika skuli hizi zinaendelea sambamba na maslahi ya walimu kama ilivyo kwa walimu wa skuli nyengine.

Pendekezo la 7
Bajeti ya vyuo vya elimu ya juu iongezwe kwa kuvipatia vyuo ruzuku au fedha za maendeleo, ili vikamilishe programu zake mbali mbali, ambazo nyingi haziwezi kusubiri mpaka hali ya fedha iwe nzuri sana mfano ujenzi wa mabweni na mpango wa kuanzisha shahada ya kwanza ya masomo ya ufundi kwa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST)

Utekelezaji
Bajeti ya Mwaka wa fedha 2017/2018 **i**kilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 imeongezeka kwa asilimia 34.

Taasisi ilidhamiria kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 iwe imeshaanza masomo ya Shahada ya kwanza ya masomo ya ufundi kupitia Idara zake ikiwa ni utekelezaji wa Mpango Mkakati wa 2015 – 2020.

Katika matayarisho ya utowaji wa mafunzo ya Shahada ya Kwanza, Taasisi iliweza kuongeza idadi ya wakufunzi wenye Shahada ya Uzamili kutoka 13 mwaka 2009 hadi 31 mwaka 2017. Katika kutimiza lengo hili ilikuwa kila Idara kuwe na wakufunzi wenye Shahada ya Uzamivu kwa ajili ya kusimamia tafiti. Kwa sasa Taasisi inahitaji kupata ufadhili au mikopo ili kuwawezesha Wakufunzi angalau watano kwa kila Idara kupata mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (PhD).

Taasisi imeanza mikakati ya kumuwezesha angalu mkufunzi mmoja kwa mwaka huu kuanza mafunzo ya Shahada ya Uzamivu nchini Malaysia.

Mafunzo ya Shahada ya Kwanza yalioanza mwaka huu, yamepata changamoto ya mabadiliko ya utaratibu wa usimamizi wa Taasisi zilizokuwa zikisimamiwa na NACTE kusimamiwa na TCU ambapo NACTE iliruhusu Mkufunzi mwenye Shahada ya Kwanza kufundisha mpaka "NTA Level 7". Baada ya mabadiliko wakufunzi wetu ambao walishatayarishwa na wanafani za mambo ya ndege walizuiwa kufundisha.

Pendekezo la 8
Majengo na miundo mbinu ya vyuo ikarabatiwe ili kuimarisha mazingira ya usomeshaji. Aidha Bodi ya mikopo ya Elimu ya Juu, inahitaji kupatiwa jengo la kutosha la kukidhi mahitaji ya kiofisi hasa uhifadhi wa kumbukumbu za wakopaji, jengo linalotumika sasa na Bodi hiyo ni finyu mno hata ukumbi wa mikutano hamna

Utekelezaji
Wizara katika kuhakikisha inaimarisha mazingira ya usomeshaji katika vyuo inaendelea na ujenzi wa maabara ya kusomea na ukumbi wa mikutano katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), utanuzi wa Taasisi ya Maendeleo ya Utalii Maruhubi (ZIToD) na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST). Aidha Wizara ikishirikiana na Serikali kuu ina mpango wa kutafuta eneo la ujenzi wa ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na bahati nzuri sana eneo hilo tayari tunalo katika eneo letu la Mazizini ilipo Makao Makuu ya Wizara.

Pendelezo la 9
Walimu wa vyuo wapatiwe maslahi yanayostahiki na nyumba za kuishi au nyezo za usafiri wa uhakika ilikuwawezesha kufanya kazi zao vizuri

Utekelezaji
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeongeza mishahara kwa wafanyakazi wote, mwezi wa April 2017, walimu nao ni miongoni mwa wafanyakazi hao. Kwa hivyo maslahi yao yameimarishwa tayari. Pia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewapatia nyumba walimu saba (7) wa Chuo cha Kiislamu Unguja katika eneo la Mazizini.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inampango wa kununua gari kwa ajili ya Vyuo vya Kiislamu Unguja na Pemba ili kurahisisha utendaji katika vyuo husika.

Kwa usafiri wa mwalimu mmoja mmoja, Wizara imetoa fursa ya mikopo katika taasisi za fedha na jumuiya tofauti zinazotoa fursa ya mikopo. Jumla la ya walimu saba (7) wamepatiwa mikopo hiyo. Walimu 3 wamekopa gari na 4 vespa.

Pendelezo la 10
Dakhalia za wanafunzi ziimarishwe na huduma za dakhalia zipatikanwe ili wanafunzi wasome katika mazingira yenye utulivu.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuimarisha dakhalia zilizopo Mazizini na katika mwaka 2018 ishaallah dakhalia hii itaanza kutowa huduma kwa wanafunzi wa sekondari ya juu wanawake vile vile Fidel castro, Utaani, CCK Micheweni, Juma Pindua, Kengeja Ufundi na KIST, pia Wizara inahakikisha inaweka mazingira mazuri ya dakhalia hasa kwa watoto wa kike.

Pendelezo la 11
Mgogoro kati ya wanajamii wa Micheweni na Chuo cha Kiisilamu Micheweni upatiwe ufumbuzi wa kudumu ili ujenzi wa chuo uendelee

Utekelezaji
Eneo la Chuo cha Kiisilamu Michweni limepimwa na lina hati miliki na tayari wananchi wamelipwa fidia ya vipando vyao, lakini wananchi hao wamelivamia tena eneo hilo na kusababisha mgogoro kuendelea. Wizara kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya inahahakisha mgogoro huu utapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Pendekezo la 12
Serikali ibuni vyanzo vya kupata fedha za kuwakopesha wanafunzi wa elimu ya juu, ambao wengi wao wanasifa za kuendelea, lakini wanakosa mkopo kutokana na uhaba wa fedha. Utaratibu wa kurejesha mikopo uende sambamba na kiasi cha mshahara wa mkopaji na hali ya uchumi, wapo wanafunzi waliokopa na wanalalamika makato ya mikopo yao ni mikubwa wakati mishahara yao ni midogo na hali ya maisha ikiwa ni ngumu.

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti, mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya juu inatolewa kulingana na vipaumbele vya SMZ. Vipaumbele hivyo vinapangwa na Tume ya Mipango Serikalini.

Wanafunzi wanaopatiwa mikopo kwa mwaka ni kati ya asilimia 30 - 40 ya waombaji wa waombaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (BMEJZ).

Kwa mwaka 2017/18 SMZ imeongeza fedha za bajeti kutoka TZS6.1B mwaka 2016/17 hadi TZS10. 2B kwa mwaka 2017/2018.

Aidha Serikali imezuwia wafanyakazi walioajiriwa na SMZ na SMT wasipatiwe mikopo kuanzia mwaka 2017/18. Lengo la kuchukua hatua hizo ni kuongeza wigo wa nafasi za kutoa mikopo na kuhakikisha wanafunzi wenye sifa wanapatiwa mikopo ili waendelee na masomo ya Vyuo vya Elimu ya Juu.

Jumla ya wanafunzi 1,600 wapya wanatarajiwa kupatiwa mikopo kati ya wanafunzi 2,675 waliotuma maombi ya mikopo kwa mwaka huu wa fedha. Mapendekezo ya kutafuta njia mbadala za kukuza mfuko wa elimu ya juu yamepokelewa na yanaendelea kuwafanyiwa kazi. Viwango vya marejesho ya mikopo vinavyotumika hivi sasa viliwekwa tangu Julai, 2012 na hadi sasa havijabadilishwa pamoja na kuwa na mishahara imebadilishwa mara tatu. Mikopo inayorejeshwa bila ya kuweka riba ili kupunguza mzigo kwa wakopaji, pamoja na kuwa *purchasing power* ya fedha inarejeshwa inapungua kwa kila mwaka. Muda wa kulipa deni unategemea na kiwango cha mkopo lakini ni kati

ya miaka minane badala ya chini ya milioni kumi mpaka kumi na sita deni la chini ya milioni thalathini na mia miaka 30 kwa deni la chini ya milioni 65. Kwa hivyo, wakopaji wenye madeni milioni 100,000,000 ambao mikato yao hupangwa kwa mujibu wa muda wao wa utumishi uliobakia kabla ya kustaafu. Bodi inafikiria utaratibu mzuri zaidi za kulinda thamani ya fedha iliyokopeshwa, uwezekano wa marejesho halisi na pia kuangalia uwezo wa mlipaji.

Pendekezo la 13. Vyuo vya Mafunzo ya Amali na vituo vya elimu mbadala vimepatiwa fedha za kutosha za kuendesha programu zao na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na mazoezi ya wanafunzi. Kamati inashauri sana fedha za *Skills Development Levy* (*SDL*) zilizotungiwa sheria na Baraza lako tukufu ambazo zinakusanywa kwa michango ya vyuo vyenyewe hasa vya binafsi zipatikane na kupatiwa vyuo vya amali na vituo mbadala. Kamati imebaini kuwa fedha hizo hazijawahi kutolewa na vyuo hata mara moja.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, fedha za kuendeleza ujuzi (*SDL*) zimepatikana katika mwaka huu wa fedha 2017/2018. Tunashukuru sana Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza lako tukufu pamoja na Wizara ya Fedha pamoja na Wawakilishi kwa kutoa msukumo ambao umepelekea kupatikana kwa fedha hizo. Jumla ya shilingi bilioni 5,497,300,000/- zimetengwa ikiwa shilingi bilioni 1,082,100,000/- kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 4,45,200,000/- kwa matumizi mengine ya ofisi. Jumla ya shilingi 301,864,000/- zitapelekwa vituo vya binafsi vinavyotoa mafunzo ya amali vilivyosajiliwa mara tu baada ya kukamilika kwa muongozo wa utoaji wa fedha hizo ambao kwa sasa upo katika mchakato wa kukutana na wadau wa mafunzo ya amali kwa kupokea michango na marekebisho.

Pendekezo la 14. Majengo na miundombinu ya vyuo na vituo vya amali yafanyiwe ukarabati ili mazingira ya kusomea yawe mazuri hasa kituo cha Forodhani ambacho hali ya majengo yake ni chakavu na kamati inapendekeza mpango ufanyike wa kujengwa majengo mengine.

Utekelezaji

Ukarabati wa banda la Karakana katika kituo cha elimu mbadala Rahaleo umeanza kwa hatua ya kupandisha matofali na kiasi cha fedha 2,465,000/- ambazo zilipatikana katika harambee ya kuadhimisha miaka kumi ya Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo zimetumika kwa ujenzi huo. Hatua inayofuata ni kazi ya uwezekaji wa banda hilo ambalo linasaidia wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri.

Aidha, wizara imetenga kiasi cha shilingi 7,852,000/- kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Forodhani na Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo.

Pendekezo la 15. Juhudi za lazima na za makusudi zifanywe kujenga uzio wa dakhalia ya wanafunzi katika Chuo cha Amali cha Vitongoji kwa ajili ya kulnda usalama wao kutokana na vitendo vya baadhi ya watu wanaovamia nyakati za usiku.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka imejipangia kujenga uzio wa vituo kwa awamu katika mwaka huu wa fedha, lakini imeweka kipaumbele katika dakhalia za wanawake za Mkokotoni na Vitongoji kuweka uzio wa senyenge, hatua za ujenzi wa ukuta zitafanyika baadae. Aidha, ujenzi wa ukuta katika Kituo cha Mafunzo ya Amali Mwanakwerekwe utaanza ndani ya robo ya mwaka Oktoba hadi Disemba.

Pendekezo la 16. Maslahi ya walimu ya vyuo na vituo vya amali yaimarishwe kwa kuwa wanajitolea sana kusomesha wanafunzi kazi za vitendo ambazo ni ngumu na zina changamoto mbali mbali. Aidha, vyuo vipatiwe usafiri wa kazi tofauti za ufatiliaji.

Utekelezaji

Mamlaka imepokea ushauri na imeshaanza kulifanyia kazi suala hili ikiwemo mchakato wa kuwapatia wafanyakazi bima ya afya. Aidha, mamlaka tayari imeshatayarisha na imeshakabidhi muundo wa taasisi na muundo wa utumishi sehemu husika kwa hatua za juu. Pia mamlaka ipo katika hatua za kukamilisha muundo wa mshahara kwa ajili ya kukuza kiwango cha mishahara ya wakufunzi. Katika bajeti ya mwaka 2017/2018 mamlaka imepanga kununua gari 5 na vespa 2 kwa ajili ya kupunguza tatizo la usafiri katika ofisi zake la vituo. Kwa sasa mamlaka imekodi basi kwa ajili ya usafiri wa walimu wanaoishi mbali na Kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni na kwa upande wa Pemba mamlaka inaendelea na utoaji wa nauli kwa wafanyakazi.

Pendekezo la 17. Wanafunzi wapatiwe nyenzo za kufanyia mazoezi. Kamati inalishauri Shirika la Bima la Zanzibar kusaidia kuwapatia Chuo cha Amali cha Mkokotoni gari zilizoharibika kwenye ajali ili wanafunzi wafanye mazoezi ya ufundi ya ukarabati wa gari hizo.

Utekelezaji

Uongozi wa mamlaka umeupokea ushauri huo na itafanya juhudi za makusudi kuwasiliana na uongozi wa Shirika la Bima ili kuona mamlaka itaweza kulifanyia kazi suala hili.

Pendekezo la 18. Baraza la Mitihani la Zanzibar ilipewa jukumu kikamilifu kusimamia mitihani ya *MOCK* ili kuwe na utaratibu mmoja tu utaodhibiti mapungufu katika mitihani hiyo. Aidha, fedha za bajeti zipatikane mapema ili Baraza lipange ratiba ya mitihani kwa wakati.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, mitihani ya *MOCK* ndio inayohusisha wanafunzi wa kidato cha nne na sita kwa Zanzibar. Kwa mujibu wa utaratibu wa mitihani ya Baraza la Mitihani la Taifa (*NECTA*), mitihani ya Kidato cha Nne na Sita husimamiwa moja kwa moja na Maafisa wa Elimu Mikoa. Kwa hivyo, mitihani ya *MOCK* nayo inasimamiwa moja kwa moja na Maafisa Elimu Mikoa. Hata hivyo, wizara itashirikiana na taasisi husika kuhakikisha

kuwa kasoro zinazojitokeza katika uendeshaji wa mitihani hiyo ya *MOCK* zinarekebishwa ipasavyo.

Aidha, ratiba za mitihani ya Taifa ya SMZ zinatoka mapema kwa mwaka huu wa 2016/2017 wizara ilipatiwa fedha zote zilizohitajika kwa shughuli za mitihani kwa wakati na kazi zote zilimalizika kwa wakati. Na hata walimu ambao walihusika na zoezi hilo walilipwa kwa wakati.

Pendekezo la 19. Changamoto za kusimamia mitihani na kambi ya kusahihisha mitihani zipatiwe ufumbuzi kwa kuwa hayo yanawezekana ndani ya wizara yenyewe.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, katika kupunguza changamoto ya usimamizi na usainishaji wa mitihani, wizara ina mipango ifuatayo.

i) Kupanga usimamizi wa mitihani kwa Wilaya badala ya usimamizi wa Mkoa kama ilivyo hivi sasa.
ii) Kuweka vituo vya usahihishaji zaidi ya kimoja kutokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya watahiniwa kwa mwaka huu tulionao.

Pendekezo la 20. Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ichukue hatua kukaa na Jeshi la Polisi kuelezana utaratibu thabiti wa hatua za kisheria kwa wale wote wanaokamata wakiiba na kuuza vitabu vya serikali, pia inashauri maktaba ipatiwe usafiri na vifaa vya kompyuta kwa upande wa Pemba.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, wizara itashirikiana kikamilifu na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika utekelezaji wa pendekezo hili. Hatua za kuimarisha huduma za usafiri na upatikanaji wa kompyuta kwa Shirika la Huduma za Maktaba Pemba zitachukuliwa katika mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Pendekezo la 21. Vituo vya Walimu (*TC's*) vipatiwe fedha za bajeti ili shughuli zao ziweze kufanyika kwa ufanisi badala ya kutegemea michango ya walimu na wazee ambao haipatikani kwa ukamilifu. Aidha, vituo vipatiwe usafiri wa uhakika viweze kufatilia walimu katika skuli zao.

Utekelezaji

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejipanga kuvipatia ruzuku vituo vya walimu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika robo ya kwanza wizara imepanga kuvipatia fedha vituo saba vya walimu, vituo vyenyewe ni Mkwajuni, Saateni, Dunga, Muwanda, Kitogani, Chachani na Michakaini. Kila kituo kimepangiwa shilingi milioni 1,000,000/-. Idara itaendelea kuvipatia fedha vituo vyote kadri ya hali itakavyokuwa inaruhusu.

Ili kupunguza tatizo la usafiri kwa washauri wa masomo katika vituo vya walimu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imepanga kununua vespa tano kwa ajili ya washauri hao kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Pendekezo la 22. Wizara iweke bajeti ya kutosha na kuhakikisha kuwa ukaguzi unfanyika mara kwa mara kwa ajili ya kujua uwezo wa walimu katika kazi zao na kurekebisha makosa kwa wakati.

Utekelezaji

Katika kuhakikisha kuwa ukaguzi unafanyika mara kwa mara ili kujua uwezo wa walimu katika kazi na kurekebisha kasoro zinazozijitokeza kwa wakati, wizara imeongeza bajeti ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kutoka shilingi 60,000,000/- kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi shilingi 120,000,000/- kwa mwaka wa fedha 2017/2018, sawa na ongezeko la asilimia 100. Kutokana na ongezeko hili ofisi itaweza kutekeleza ukaguzi wa kanda na imepanga kuzikagua skuli 518 (286 Unguja na 232 kwa Pemba).

Pendekezo la 23. Kwa kuwa elimu ndio mkombozi wa Taifa na maendeleo, serikali ihakikishe inaongeza bajeti yake kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kuhakikisha kuwa kasma inayopangwa na OC zinapatikana tena za kutosha, kwa ajili ya shughuli muhimu pamoja na kazi zinazotaka kutekelezwa zisikwame.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaipongeza sana serikali kuu kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuchagua wizara yetu kuwa miongoni mwa wizara nne zilizoingiziwa fedha zote za *OC* za robo ya mwaka ya Julai hadi Septemba. Hali hii itasaidia wizara kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa. Aidha, utaratibu huu ukiendelea kwa kila robo mwaka ufanisi wa kazi utapatikana kulingana na mpango uliowekwa.

Pendekezo la 24. Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iwe makini katika kutafuta wakandarasi na washauri elekezi juu ya miradi ya ujenzi na katika miradi yenye ufadhili yawepo majadiliano ya pamoja na wafadhili wa miradi hiyo katika kuweka vigezo vya kupata wakandarasi na washauri elekezi ambao hawatachelewesha kukamilika kwa miradi ya ujenzi.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, wizara kupitia Kitengo cha Manunuzi na Ugavi inaweka na kuzingiatia vigezo (masharti) mbali mbali ambavyo vinazingatia sheria mpya ya manunuzi na taratibu kama zimepangwa na sheria ya manunuzi ya mwaka 2016 na miongozo yake. Vile vile kwa miradi ya wafadhili, wizara imefanya majadiliano na wafadhili hao kwa kila hatua na *No Objection*.

Pendekezo la 25. Mhe. Mwenyekiti, mkakati maalum wa kuhakikisha skuli zinapata walimu bora wa sayansi, upangwe kwa kuongeza maslahi zaidi, na kuwapatia mafunzo

walimu na mbinu bora za ufundishaji walimu waliopo sasa. Mpango huu pia utafanikiwa kwa kupatiwa fedha, nyenzo pamoja na usafiri kwa vituo vya walimu (*TC's*).

Utekelezaji

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeendesha mafunzo mbali mbali kwa walimu wa Sayansi na Hesabati katika ngazi zote kwa ajili ya kukuza uwezo wa ufundishaji kwa walimu hao. Miongoni mwa mafunzo hayo ni kama ifuatavyo.

i) Mbinu za ufundishaji wa mada ngumu kwa walimu wa madarasa ya msingi juu. Jumla ya walimu 900 walishiriki mafunzo hayo.
ii) Matumizi ya vifaa vya Sayansi na Hesabati kwa walimu wa msingi na sekondari.
iii) Matumizi ya mbinu ya ufundishaji wa kutumia picha. Mafunzo hayo yametolewa kwa wakufunzi 40 wa Chuo cha Kiislamu 75, walimu 35 wa skuli za Mwera na Kiembesamaki A na B. Pia mafunzo kama haya yatafanyika kwa wakufunzi wa Chuo cha Kiislamu Pemba kati ya mwezi Januari, 2018.

Washauri wa masomo wanapotembelea skuli walimu hupata taaluma ya ziada kutoka kwa washauri hao juu ya mbinu na hata matumizi ya zana za kufundishia. Ili kukuza uwezo wa walimu zaidi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendesha mafunzo kwa walimu 2,500 wa masomo ya Sayansi na Hesabati katika mwaka wa fedha 2017/2018 – 2019/2020 kupitia wafadhili wa Benki ya Dunia.

Pendekezo la 26. Serikali itafute wafadhili kujenga maktaba katika kila Mkoa ili kutanua wigo wa kujiongezea maarifa.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wizara ina mpango wa kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kujenga maabara na maktaba katika skuli 23, skuli 14 Unguja na skuli 9 Pemba kwa kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia. Majengo hayo yatajengwa katika skuli za Jang'ombe, Kisauni, Tumbatu, Kijini, Mkwajuni, Donge, Mahonda, Chuwini, Kitope, Mtoni, Kigomeni, Uroa, Regeza mwendo, Unguja Ukuu, Bwejuu, Kiuyu, Makangale, Kisiwa Panza, Mtambile, Kilindi, Pujini, Kojani, Fundo na Limbani.

Pendelezo la mwisho ambalo ni la 27. Serikali itoe fursa za ajira kwa wakutubi na wasaidizi maabara katika skuli za sekondari badala ya kutumia walimu wa kawaida kufanya kazi hizo, huku walimu hao wakiwa na vipindi vya kusomesha madarasani.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano imepanga kuajiri wakutubi 123 na wafanyakazi wa maabara 555. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wizara imewasilisha Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora mahitaji ya wakutubi 25 na wafanyakazi wa maabara 100 kwa hatua zao kwa utekelezaji wa awali.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, napenda tena kutoa shukurani za dhati kabisa kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza lako tukufu kwa ushauri wao, maelekezo na mashirikiano ya pamoja. Pia niwaombe sana wajumbe wako wote waendelee kushirikiana na sisi kama ambavyo wanaendelea kufanya siku zote na kwa hili tunawashukuru sana kwa mashirikiano ambayo wanatupatia kuona changamoto nyingi za elimu tumeweza kuzitatua kwa pamoja na kwa haraka zaidi. Mashirikiano yetu ya pamoja yatazidi kunyanyua maendeleo ya elimu ndani ya nchi yetu. Elimu bora kwanza kwa wote inawezekana sana pale ambapo tutashirikiana kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa taarifa yako ya utekelezaji, sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwasilisha Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati wa Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Kuhusu Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kuendeleza kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Aidha, nachukua nafasi hii adhimu kwa moyo wa dhati kabisa, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusiana na utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuendeleza vizuri sera za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kutoa elimu bila malipo. Tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inatekeleza agizo lake la kuzuwia michango katika skuli za msingi. Hivi majuzi tu Mhe. Rais tarehe 23/9/2017 kule Gombani, Pemba katika sherehe za Elimu bila Malipo aliahidi kwamba, kuanzia mwaka ujao wa fedha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itasitisha michango katika skuli zote za Sekondari za Serikali Unguja na Pemba.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mhe. Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Riziki Pembe Juma pamoja na Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri pamoja na watendaji wao wote kwa jitihada zao mbali mbali wanazozichukua katika kuhakikisha kwamba sekta ya elimu inasonga mbele kwa mujibu wa malengo ya kitaifa (MKUZA III) na malengo ya maendeleo endelevu *(Sustainable Development Goals)*.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Ustwai wa Jamii kwa michango yao mikubwa waliyoitoa wakati wa uwasilishwaji wa utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa Ripoti iliyopita. Lengo kubwa la michango hiyo ni kuhakikisha kuwa sekta ya elimu inasonga mbele pamoja na kuzitatua changamoto mbali mbali zinazoikabili sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii niwatambue wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame	Mwenyekiti
2.	Mhe. Tatu Mohammed Ussi	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Hidaya Ali Makame	Mjumbe
4.	Mhe. Makame Said Juma	Mjumbe
5.	Mhe. Masoud Abrahman Masoud	Mjumbe
6.	Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Mjumbe
7.	Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Mjumbe
8.	Ndg. Aziza Waziri Kheir	Katibu
9.	Ndg. Khamis Hamadi Haji	Katibu

UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA RIPOTI YA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, **k**amati ilikutana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tarehe 11/9/2017 na kupokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya kamati kama yalivyoagizwa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka 2016/2017. Aidha, kwa kiasi kikubwa kamati imeridhika na utekelezaji wa yale yaliyoagizwa, ambapo mengi miongoni mwa maagizo hayo yana lengo la kuisaidia serikali na wizara kwa ujumla kunyanyua kiwango cha elimu nchini mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji huo, kuna baadhi ya changamoto bado hazijatatuliwa mpaka sasa, jambo ambalo linaendelea kuwa ni kikwazo kwa baadhi ya skuli na kuwepo maendeleo endelevu ya elimu ya watoto wetu. Baadhi ya changamoto hizo ambazo bado hazijapatiwa ufumbuzi ni kama ifuatavyo:-

UKOSEFU WA MAABARA KWA BAADHI YA SKULI PAMOJA NA VITENDEA KAZI

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa maagizo ya kamati ni pamoja na suala la maabara za uhakika katika skuli za sekondari zenye kufundisha masomo ya sayansi pamoja na vitendea kazi. Ingawa Mhe. Waziri tunamshukuru katika kujibu ameeleza ambazo serikali inaendelea kuchukua.

Katika kupokea utekelezaji wa maagizo, kamati iliridhishwa na jitihada zinazochukuliwa na serikali za kutatua changamoto ya maabara za uhakika pamoja na vitendea kazi. Hata hivyo, suala hili bado halijakaa sawa kwa baadhi ya skuli nyingi za serikali ambazo zinafundisha masomo ya sayansi kutokana na kukosekana kwa vitendea kazi na baadhi ya wakati kuchelewa kuapatikana kwa nyenzo hizo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili limekua ni changamoto kubwa na linarudisha nyuma juhudi za walimu pamoja na watoto wetu ambao kwa sasa wamekua na mwamko mkubwa wa kusoma. Hivyo, kamati inazidi kuisisitiza wizara pamoja na serikali kwa ujumla kujidhatiti kuzipatia vitendea kazi kwa wakati maabara zote ili wanafunzi wetu wapate kujifunza kwa vitendo, kwa mapana zaidi na kuweza kufaulu kwa viwango vya juu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inazidi kusisitiza kuwa, Wizara na Serikali kwa ujumla ifanye juhudi ya kuajiri *"Lab Technicians"* kwa kila maabara kwa kuwasaidia walimu wa sayansi ili kuwe na ufanisi mzuri wa kazi. Kamati inashauri endapo serikali itaona kuna haja ya kujenga maabara mpya na za kisasa, basi ifanye utaratibu wa kujenga maabara chache kwa kuanzia zilizokamilika, ambazo zitakua na vifaa vyote vinavyopaswa kuwepo katika maabara pamoja na wafanyakazi wa kutosha *(Lab technicians)*. Suala la msingi pia ni upatikanaji wa vitendea kazi (*apparatus*) na Kemikali (*reagents*) kwa masomo ya vitendo kwa wanafunzi.

Maabara hizo, zitatumika kwa wanafunzi pale wanapohitaji kujifunza kwa vitendo. Maabara hizo kwa kuanzia tunashauri zijengwe kiwilaya.

UAJIRI WA WALIMU PAMOJA NA KUREKEBISHWA KWA MUUNDO WA UTUMISHI WA WALIMU

Mhe. Mwenyekiti, suala la uajiri wa walimu hasa wa sayansi ni miongoni mwa changamoto kubwa ambayo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakabiliana nayo. Pamoja na maelezo yaliyotolewa kwa kamati yetu, naomba kuisisitiza wizara kuona umuhimu wa kuajiri walimu wengi kwa lengo la kuondoa changamoto kubwa iliyopo hivi sasa pamoja na kurekebisha muundo wa utumishi wa walimu *(Scheme of Service)*.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaiomba wizara kutoa kipaumbele cha kipekee kwa walimu wa Vyuo vya Amali kwa kuwaajri wa kutosha ili kuwapa taaluma vijana wetu ambao wengi wao hutegemea taaluma wanayopatiwa kwa kujiajiri na kuendesha maisha yao.

Aidha, kamati inachukua nafasi hii, kuiomba tena Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na muongozo iliyoutoa, kuziangalia fani maalum zikiwemo za walimu wanaofundisha vyuo vya mafunzo ya amali kwa kuwapa kipaumbele cha kuwaongezea ujuzi kwa kuwasomesha kwa fedha za serikali na sio kujisomesha kwa fedha zao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inasisitiza suala la kuangaliwa kwa muundo wa utumishi wa walimu kutokana na ukweli kwamba, kamati ilipofanya ziara katika kazi zake za kawaida ilikutana na changamoto kubwa kutoka kwa walimu wengi kutaka kustaafu kabla ya muda wao wa kustaafu kufika, jambo ambalo endapo litafanyika skuli nyingi za serikali zitakosa walimu wengi wazoefu ambao ni chachu ya maendeleo ya elimu kwa watoto wetu.

Sababu yao kubwa ya kutaka kustaafu mapema ni kutoridhika na marekebisho ya mishahara ambayo wanahisi haayakuwanufaisha kulingana na uzoefu walionao wa miaka mingi.

SUALA LA KUJENGA UZIO KATIKA MAENEO YA SKULI NA VYUO PAMOJA NA KUPATIKANA HATI MILIKI ZA MAENEO

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu ilipokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo ambapo baadhi ya skuli na vyuo zinazoguswa na agizo hili bado matatizo yanaendelea. Miongoni mwa maeneo yanayokabiliwa na tatizo la uvamizi wa maeneo yao ni pamoja na eneo la Chuo cha Kiislamu Micheweni, ambapo kamati ilielezwa kwamba maeneo ya chuo hicho tayari yameshapimwa na tayari hati miliki zake zipo.

Hata hivyo, kuna baadhi ya wananchi wameyavamia tena maeneo hayo pamoja na ukweli kwamba wameshalipwa fidia zao. Aidha, kamati ilielezwa kwamba, wizara kwa kushirikiana na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Mkuu wa Wilaya ya Micheweni itahakikisha mgogoro huo unapatiwa ufumbuzi wa kudumu, ukweli suala hilo limechukuwa muda mrefu kutatuliwa. Pamoja na maelezo hayo, kamati inasisitiza kwamba mgogoro huo upatiwe ufumbuzi kwa namna yoyote ile ili wanafunzi wa chuo hicho waweze kusoma bila usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, migogoro mingi inayohusiana na wananchi pamoja na maeneo ya skuli na vyuo vya serikali inasababishwa na maeneo hayo kutohifadhiwa kwa kukosa uzio unaoonesha mipaka ya maeneo hayo. Ili kuepuka migogoro ya uvamizi wa maeneo ya skuli pamoja na kuweka usalama wa kutosha, kamati inazidi kusisitiza suala la ujenzi wa ukuta katika maeneo ya skuli na vyuo liwe endelevu, pamoja na hatua za awali ambazo zimeshaanza kuchukuliwa na wizara za kujenga uzio katika baadhi ya skuli na vyuo.

SUALA LA AJIRA KWA WALIMU WAPYA

Mhe. Mwenyekiti, upungufu wa walimu ni tatizo sugu kwa skuli nyingi ambazo kamati imepata fursa ya kuzitembelea kote Unguja na Pemba. Upungufu huu huu unahusisha zaidi walimu wa fani mbali mbali husasan wa masomo ya sayansi, ambapo kila skuli tuliyotembelea kilio ni kikubwa. Kamati ya Ustawi wa Jamii inapongeza juhudi zinazochukuliwa na serikali kwa kuanzia kukabiliana na upungufu huu kwa kuajiri walimu wapya hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizo, kamati yangu inaiagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya utafiti wa kina utakaobainisha mahitaji halisi ya walimu kwa skuli za Unguja na Pemba na kukabidhi serikalini ili wizara inayohusika na Utumishi wa Umma itakapotangaza nafasi za ajira kwa walimu waweze kujua mahitaji halisi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inashauri pia serikali kuhakikisha nafasi mpya za ajira zinapatikana kila mwaka kwa kuwa kila mwaka kuna walimu wanaostaafu. Kwa hivyo, nafasi tupu zinakuwepo na zinatakiwa zijazwe bila ya kungoja na muda kupita.

KUONGEZA IDADI YA WANAFUNZI KATIKA VYUO VYA ELIMU YA JUU

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa kuiongezea bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, jambo ambalo limeongeza idadi ya wanafunzi wanaopatiwa mikopo kwa mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, kamati yetu inachukua nafasi hii kutoa rai na kuishauri wizara kwa kushiurikiana na Bodi ya Mikopo kufanya juhudi za kuwaomba wafanyabiashara wakubwa waliopo hapa nchini ambao watakua tayari kuwasaidia wanafunzi wetu kwa kuwakopesha fedha kwa makubaliano maalumu yatakayokuwa na unafuu wa kurudisha mikopo hiyo, ili idadi ya wanafunzi watakaosomeshwa kwa kupatiwa mikopo izidi kuongezeka. Kwa mara nyengine tena tunaiomba sekta binafsi kuchangia Mfuko wa Mikopo wa Elimu ya Juu. Suala hili limeweza kutekelezwa vyema katika nchi kadhaa kwa mfano Singapore, Malaysia na kwengineko.

SUALA LA WIZI WA VITABU VYA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii ilitoa agizo kwa wizara kushirikiana na Ofisi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa lengo la kukomesha wizi huo kwa kuwafikisha wanaohusika na wizi wa vitabu hivyo katika vyombo vya kisheria. Hata hivyo, agizo hili bado halijatekelezwa mpaka sasa. Kwa mnasaba huo, kamati inasisitiza utekelezwaji wa agizo hili kutokana na upotevu wa vitabu vingi ambavyo ni mali ya serikali. Aidha, kamati inaiagiza wizara kukutana na Kamishna wa Polisi Zanzibar kwa lengo la kulitafutia ufumbuzi tatizo hili ambalo linaonekana kushika kasi na kuwa sugu.

KUHUSIANA NA SUALA LA TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJI (*KIST*) KUHUSU UMEME WA *SOLAR*

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ilipewa changamoto kubwa iliyopo katika Taasisi hiyo ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ya matumizi ya umeme wa *Solar*, ambapo taasisi hiyo ilifanya jitihada zake wenyewe kuzalisha umeme ambao unatumika katika matumizi mbali mbali hapo chuoni. Hata hivyo, kamati ilipewa taarifa kwamba, Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*) lilifika chuoni hapo na kuitaka taasisi hiyo ilipie umeme huo ambao wameuzalisha kwa ubunifu wao wenyewe na juhudi zao binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, kamati iliagiza suala hilo lishughulikiwe kiwizara baina ya wizara mbili, (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira) kwa lengo la kuweka makubaliano maalumu kuhusiana na matumizi ya umeme huo, hasa ikizingatiwa kwamba umeme huo unatumika katika Taasisi ya Elimu ys Serikali na kuwapatia mafunzo wataalamu wetu wa baadae.

Mhe. Mwenyekiti, hivi kweli taasisi mbili za serikali zenye lengo la kuwatumikia wananchi
zinashindwa kukaa pamoja kuzungumzia suala la manufaa kwa nchi yetu?

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa kumalizia kwa ujumla Kamati ya Ustawi wa Jamii imeridhika na kiasi kikubwa cha utendaji kutokana na utekelezaji wa yale iliyoyaona wakati wa ziara za kamati na kuyaagiza kwa wizara kwa ajili ya utekelezaji wao ambao utaleta tija katika sekta ya elimu na kunyanyua viwango vya elimu kwa vijana wetu. Kutokana na utekelezaji huo, kamati inachukua nafasi hii kuipongeza tena Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na serikali kwa ujumla kwa juhudi zake mbali mbali inazochukuwa katika kuzitatua changamoto zilizopo, tunaomba juhudi hizi ziwe endelevu ili hatimaye kuweza kumaliza changamoto nyingi kama si zote zinazoikabili sekta ya elimu.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza haya naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na kwa makini na naaomba watoe michango yao katika ripoti hii ya utekelezaji ya Wizara ya Elimu kushauri inavyopasa na hatimaye kuipokea ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti**,** mwisho kabisa nakushukuru wewe kwa kunipa wasaa huu wa kuwasilisha ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini, Mwakilishi wa Jimbo la Dimani, lakini pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa hotuba yako. Sasa Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea na nitamwita mchangiaji wa kwanza Mhe. Ali Suleiman Ali na kama muda utaruhusu kwa sasa atafuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Makamishna. Aidha, Walimu Wakuu, walimu wote pamoja na wanafunzi kwamba wao ni changamoto moja ya kuendeleza wizara hii juu ya kupata mafanikio ya elimu katika nchi yetu.

Pia Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze Wazanzibari wote kwa kujua kwamba thamani ya elimu hailipiki na haina kiasi. Kwa hivyo, tuwaunge mkono walimu na kamati za wazazi katika skuli zetu ili kuendeleza elimu vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa makusudi nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein hasa kwa kuzingatia yale ninayosema kila siku kila zuri inabidi ulipongeze na kila zuri uliige. Kwa sababu mimi niliyesimama hapa namshukuru Mwenyezi Mungu toka nimesoma darasa la mwanzo mpaka nimemaliza sekondari sikuchangia hata shilingi 100 katika masomo yangu. Kwa hivyo, wakati huo Marehemu Rais wetu wa mwanzo Mzee Abeid Amani Karume ndio sera yake mara baada ya Mapinduzi aliweka hivyo. Lakini na waliofuatia pia

wametekeleza hayo na kwa kiwango kikubwa tumpongeze Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuhakikisha kwamba ile mizizi yote iliyokuwa ina kasoro kaiondoa sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ni ngumu kuipata lakini pia kama unamsomesha mtoto wako ni suala gumu sana. Kwa hivyo kama Mhe. Rais kaona pana haja kwamba elimu ya msingi kuanzia darasa la kwanza mpaka la sita bure hilo ni suala kubwa sana. Lakini badala yake katika sherehe ya mwaka huu ya Elimu Bila ya Malipo Pemba akasema tu kwamba, pamoja na hilo alilolianzisha mwanzo pana haja ya kuwaongezea faida wananchi wake, kuwaondolea mzigo wa kuchangia elimu. Maana kuchangia elimu si jambo dogo, Mhe. Rais kwa imani yake na kwa uwezo wake na umahiri wake kasema tu kwamba Mwenyezi Mungu akitufikisha mwaka 2018/2019 bajeti ijayo kuanzia Julai, elimu ya sekondari yote bure. Kwa hivyo, tumpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa na Mwenyezi Mungu ampe hekima na serikali yetu aipe uwezo zaidi ili lifanikiwe hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya shukurani hizo zote nilizozitanguliza niseme tu kwamba naipongeza Wizara ya Elimu kupitia serikali yetu kwa kuona kila penye haja na wanafunzi au watoto wengi wanaoishi katika maeneo ya karibu basi wapate skuli ya kusomea ili waache kwenda masafa ya mbali.

Mwaka huu wa uchaguzi ulipomalizika mimi niliiomba sana serikali kuwafikiria wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele sehemu ya Kwarara. Wanafunzi hawa wanapata shida sana, watoto hao wanatoka mbali sana na kwa wakati huo ilikuwa hata barabara hakuna, lakini kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu na kwa uwezo wa serikali yetu na amri nzuri za Mhe. Rais baada ya utekelezaji nasema nimefanikiwa katika sekondari kwa asilimia mia moja. Skuli ya Kwarara, (*Tumaini Secondary School),* hii ni skuli ya mfano na kwa sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, nafikiri katika mitihani iliyofanywa safari hii wametokea watatu na hii ni changamoto tosha kusema kwamba watoto wanasoma katika mazingira mazuri, mazingira ya utulivu na walimu pia wamejipanga vizuri kuhakikisha kwamba ubora wa skuli ile na watoe wanafunzi bora na wenye uwezo katika kuendesha elimu na maisha yao ya baadae.

Mhe. Mwenyekiti, katika kulitafakari hilo mara baada ya ndugu zetu wa Korea waliposema sisi katika misaada yetu hatujengi sekondari tunajenga msingi, baada ya kuwaeleza kilio cha wananchi wa jimbo lile na sehemu hiyo wamekubali kwa makusudi katika kitabu. Kitabu hiki kipo na mimi shahidi naelewa yote kwamba wameshatia saini kuanza ujenzi wa skuli mpya ya Kwarara Msingi. Skuli hiyo Mheshimiwa namuomba sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuna utaratibu ambao unapitia kwake wale wanaotoa msaada wako tayari sasa hivi, lakini na yeye ndiye mwenye shughuli za hapa na pale, tunamuunga mkono shughuli za serikali zote ziko mikononi mwake yeye namuomba atufanyie bidii hiyo hati inayotakiwa ikamilike haraka ili ujenzi uanze. Hili sio kwa skuli ya msingi ya Kwarara tu na skuli nyenginezo mfano wanayoiita Fuoni Pangawe, Jimbo la Pangawe na hii nayo halikadhalika inasubiri hati hiyo Mheshimiwa tuanze kazi. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu hili alione kwamba anayekuthamini ndiye atakaekusaidia na asiyekuthamini hakusaidii. Kwa hivyo, natoa pongeza za dhati kabisa kwa Serikali ya South Korea na wenzetu Wachina ambao wanaelekeza katika skuli hizi na nyenginezo kusaidia watoto wetu ili twende kutokana na wingi wa wanafunzi katika madarasa wapungue.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, jengine niseme tu kwamba katika walimu mimi nawapongeza wote. Mheshimiwa walimu wana kazi nzito na wewe mmoja uliyekuwepo hapo na Waziri wa Elimu mwalimu, Naibu Waziri mwalimu, kuna Mwalimu Haroun Ali Suleiman yumo humu na wengineo wengi hata wawakilishi wengine wako huko wametokea katika fani hiyo. Kwa hivyo, niseme tu kwamba ualimu ni suala gumu na ualimu fadhila zake mwanafunzi huzilipi na kama yuko anayethubutu kusema atazilipa fadhila za mwalimu sitegemei mtu huyo kama ana akili timamu. Kwa sababu mwalimu anapokuelimisha wewe anavyokuendeleza ujue ni hatua moja sawasawa na mzee wako anaekuhudumia wewe katika maisha yako. Kwa hivyo, radhi za mwalimu ni kubwa na radhi zake ukidharau au ukienda kinyume zinakupata. Hivyo niwaombe walimu wetu waongeze kasi ya maendeleo ya kuwasomesha watoto wetu na kuwaelimisha ipasavyo.

Mimi nishukuru tu kwamba Mhe. Mwenyekiti, walimu wana mpango mzuri hasa wanawake. Walimu wanawake katika nchi yetu wanapenda sare ya kuvaa pamoja mfano hata kina mama wote tu kama pana shughuli watakwambia tupate madira ya aina fulani kwasababu wanajua huu ndio umoja wetu. Kwa hivyo, mimi nitoe wito au niiombe sana wizara walimu wetu tujue wanachokivaa kitu cha heshima mabaibui ni kitu cha heshima, lakini kuna mavazi ambayo yanapendeza mfano Mhe. Waziri wa Elimu yule pale na wengine mliokuwemo humu mitandio mizuri, mavazi yenu ya heshima na walimu tunajua anapokwenda skuli kavaa sare ambayo inaungana na skuli ile yote kwa jumla na vazi la heshima inapendeza zaidi.

Lakini mimi niombe Mheshimiwa baadhi ya skuli kuna walimu wanawanyanyasa wenzao wanaovaa nguo za sare wao wanavaa mabaibui siku nyengine wengine maninja. Mwalimu anakwenda pale kavalia siku nyengine hata uso wake huoni. Hiyo Mhe. Mwenyekiti, si maadili ya ualimu. Ualimu ukienda unatabasamu na umevaa vizuri na mwanafunzi anajua ende vizuri kufata hadhi ya mwalimu wake.

Mhe. Mwenyekiti, nasema katika skuli zetu za Unguja na Pemba asilimia 98 au 100 kabisa wengi wanawake au kina mama walimu wanapenda kuvaa sare na sare zao zinathaminika. Nimuombe sana Mhe. Waziri hili alitolee wito maalum. Maana unapokwenda kwa wengine hawa wamevaa sare yao ya skuli, hawa mabaibui uso hauonekani kidogo inatisha. Wakati humeharibika huu Mhe. Mwenyekiti. Wakati tulionao Mheshimiwa unatakiwa sura ya mtu ioneakane na ndio maana unapoingia katika maeneo fulani au maeneo yoyote siku hizi unaambiwa kwanza tuone sura yako ili ukaribishwe katika eneo lile.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, tukubali kwamba maendeleo yote yanapatikana kutokana na umoja, kina mama wakikaa pamoja wakipenda kupendana katika vazi la pamoja nafikiri hilo ni zuri zaidi na maendeleo yanapatikana zaidi kwa kasi zaidi katika eneo hili hata katika maandamano skuli fulani walimu wamevaa hichi. Najua muda umekwisha Mheshimiwa nitakaa sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa kwa kuwa muda nasema tu kwamba Mheshimiwa hayo niliyoyatoa pongezi na mambo mengineyo. Bado nampongeza Mhe. Waziri na Naibu Waziri na wizara nzima kwa jumla na walimu wakuu na walimu wote, pamoja na

kamati za skuli kwa kuhakikisha kwamba thamani hii ya Mhe. Rais wetu aliyoitoa na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atamlipa fadhila njema kabisa ziwaendeleze watoto wetu.

Baada ya hayo, Mheshimiwa naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali wa Jimbo la Kijitoupele kwa mchango wako. Sasa nitamwita mchangiaji wetu wa mwisho kwa muda muu nitampa dakika 10 Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Taarifa ya Utelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi ya Jamii. Mhe. Mwenyekiti, mimi hizo dakika 10 ni nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa kwanza inasema kwamba:

"Huduma za lazima na miundo mbinu ziimarishwe katika Skuli za Maandilizi na Msingi, upatikanaji wa huduma za lazima kama vile vyoo, maji na mambo mengine".

Mhe. Mwenyekiti, kama utakuwa shahidi ndani ya bajeti tulizungumzia hapa kuhusu upatikani wa vyoo na huduma hizi za maji maskulini. Mhe. Mwenyekiti, maskulini baadhi ya maskuli mengine katika majimbo yetu kuna changamoto hizi pindi kwa kama wizara imejitahidi sana nawapongeza kwa hilo kwa kufanikisha suala hili, hapa wamesema kwamba wamejenga vyoo 210 vikiwemo vyoo vya watoto wenye mahitaji maalum wanafunzi wale nawapongeza sana kwa hilo. Lakini niwaombe sana wazidi kuchukuwa bidii kuhakikisha kwamba huduma hizi maskulini ni muhimu sana kwa sababu panapokosekana huduma hizi maskulini wanafunzi wanakuwa na mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha katika jimbo langu Skuli ya Ziwani nilikwenda wakanipa malalamiko walimu pale kwamba hapana huduma ya maji, nikatoa shilingi milioni moja kuwatafuta watu wa Mamlaka ya Maji *ZAWA* ili kuhakikisha kwamba huduma ile ya maji Skuli ya Ziwani ipatikane. Mhe. Mwenyekiti, cha kushangaza ni kwamba uongozi wa skuli ile una kamati ya skuli Mjumbe mmoja akatoa kauli kwamba pesa yangu mimi pale kama Mwakilishi isiende. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kitu hichi cha kusikitisha kwa sababu skuli ni jengo la serikali yeye kama ni kukataa akatae kwake.

Lakini Mheshimiwa mimi nilijua kwamba Mjumbe mmoja wa kamati walimu wakuu Skuli ya Sekondari na Skuli ya Msingi ni Wajumbe katika Kamati za Skuli. Sasa lakini nilijua kwamba inawezekana mpaka hawa walimu kwa sababu haiwezekani kama Mjumbe mmoja wa Kamati apinge maendeleo ninayoyapeleka mimi Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, nikajua kwamba na walimu walisababisha hili. (*Makofi*)

Nikampa taarifa Afisa Mdhamini Pemba, Naibu Waziri wa Elimu, Mhe. Waziri wewe sijakwambie na sikutaka kuja kukwambia nikasema nije niseme humu mpaka leo hakuna hatua iliyochukuliwa. Kusema la ukweli tunavunjika moyo, tuna imani na wananchi

kuwaletea maendeleo kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini Mhe. Mwenyekiti, kusema la ukweli tunarudi nyuma kutokana na hali kama ile. (*Makofi*)

Juzi Mhe. Naibu Waziri akaulizwa kuhusu suala la siasa maskulini. Mhe. Naibu Waziri akasema kwamba hakuna. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hilo nini kama si siasa mimi napeleka pesa skuli kuhakikisha kwamba wanafunzi wapate maji pale wanafunzi wanakwenda kwao majumbani kwao kujisaidia wengine hawarudi tena maskulini, hawarudi kabisa wanakwenda kujisaidia vichakani hawarudi tunapiga kelele kila siku wanafunzi wanabakwa leo napeleka maji thamani ya shilingi milioni moja anatoka Mjumbe anasema kwamba pesa Mwakilishi siitaki isiende ile skuli si yake ni nikawambia kwamba hii skuli hujaijenga wewe nikathubutu kusema. Nikawambia kwamba hii skuli ni Skuli ya Serikali hili ni jengo la serikali nikathubutu kumwambia kwamba hii skuli si ya baba yake wala si ya mama yake hawezi kukataa. (*Makofi*)

Lakini cha kushangaza hakuna hatua yoyote na mimi nilitoa agizo kama Mwakilishi pale kwamba nikawaambia wale walimu nawapa muda wa siku 3 mniletee barua, mkae vikao vyenu mnavyovijua kwa taratibu zetu lakini Mjumbe huyu wa Skuli muweze kumfukuza katika Kamati ya Skuli. Hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa Mhe. Waziri mpaka leo hii Skuli ya Ziwani maji hayapo na walimu nikawapa agizo kwamba mtatumia kwa pesa zenu, kwa sababu mimi nimepeleka mkakataa pesa ile nikaipeleka Skuli ya Kwale. (*Makofi*)

Sasa cha kusikitisha Afisa Mdhamini nilimpa taarifa na Naibu Waziri nikamuelezea hili mpaka *DC* alieondoka nikampa hii taarifa nikachukuwa vyombo vya habari *ZBC live* na wengine waliona wakanipongeza kwa jitihada zangu. Lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Sasa nauliza Mhe. Waziri ni sababu gani iliyopelekea hadi leo hii Skuli ya Ziwani pesa niliipelekea ikakataliwa maji hayajafika na mimi nikatoa amri nikawaambia kwamba itabidi walimu mchange, mkope, mnyanganye muibe lakini maji hapa myatie kwa pesa zenu hakuna iliyochukuliwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri alichukuwe hili kwa sababu "Mwiba uchomeapo ndipo utuokeapo" nililipeleka kule halikuchukuliwa hatua nampa tena waziri nambebesha mzigo huu kuhakikisha kwamba tukimaliza kikao hichi wanafunzi wale wapate maji ili wapate kusoma vizuri wapate huduma kama inavyoendelea. Mhe. Waziri nakuomba sana hilo ulichukuwe na ulifanyie kazi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa 9 kuhusu migogoro. Kamati imesema migogoro kati ya wanajamii ya Micheweni na Chuo cha Kiislamu. Mhe. Mwenyekiti, tunashuhudia sana Maskuli yanakumbwa na migogoro na Mhe. Mwenyekiti, mimi shahidi wa hilo na kila siku napiga kelele humu Skuli ya Ndagoni tangu mwaka 1998 mpaka leo hii halijapatiwa ufumbuzi suala lile pale jengo halijapimwa Wizara ya Elimu walipewa barua hii kurudisha kwamba walitamka Mheshimiwa naomba uniruhusu niweze kusoma hii barua.

Mhe. Mwenyekiti, inasema hivi:

"Kuhusu kurejeshewa eneo la Shamba yenu lililochukuliwa na Wizara ya Elimu katika eneo lililopo mkabala na Skuli ya Ndagoni"

Mhe. Mwenyekiti, suala hili nililisema na Mhe. Waziri ni shahidi na Wajumbe wote Skuli ya Ndagoni mpaka leo hii haijapimwa mgogoro ule upo. Mhe. Waziri mkanambia kwamba mtaunda kamati na kamati ni kweli mmeunda lakini mpaka leo hii huu ni mwaka tena hakuna jibu kamati iliyoundwa. Sasa naomba tena kwa mara ya pili au kwa mara ya tatu kusema kwamba suala lile la mgogoro ya Skuli ya Ndagoni lipatiwe ufumbuzi ile skuli ile ipimwe ijulikane mikapa yake ni ipi ili hii bughuza liondoke.

Mhe. Mwenyekiti, kwani waliotoa lile eneo walitoa kwa nia njema. Lakini sasa kama kuna tatizo hilo ni tatizo la kuzungumzika huu ni mwaka wa 20 tangu Baraza lililopita lilikuwa likizungumziwa suala hili. Kwa hiyo, namuomba tena Mhe. Waziri ile kamati mlioiunda nataka majibu ya kwamba limemalizika na wale kama kuna haki yao wapewe ili kuhakikisha kwamba suala lile limemalizika.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa 15 kamati imesema mikakati maalum ya kuhakikisha skuli zinapatiwa walimu. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana Wizara ya Elimu kwa kupongeza tupongeze, lakini kwa kushauri tushauri tushauri pa kusema kwamba pafanywe hivi pafanywe. Mhe. Mwenyekiti, kama ni lengo la "Hapa kazi tu" iwe hapa "Kazi kazi".

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana Wizara ya Elimu kwa kuwaajiri walimu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, jana nilikuwa nikizungumza na Mhe. Mussa Foum wa Kiwani akanambia kwamba skuli yake katika Jimbo lake Muwambe kuna walimu Skuli ya Msingi 33 wanahitajika, hebu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri upo walimu 33 hawapo kweli patapatikana elimu hapo katika skuli haipatikani. Kwa hiyo, naomba sana yale maskuli ambayo yana uhaba wa walimu na wenye sifa hizo wapo wamesoma basi ni kwamba waajiriwe waweze kutoa elimu maskulini. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono ripoti hii lakini namuomba Mhe. Waziri kwa yale yote niliyomwambia ayafanyie kazi isiwe kila siku tunasuguana humu, tunasukuma kwa suala hilo hilo moja, suala la kuondoshwa liondoshwe na suala la kufanyiwa kazi lifanyiwe kazi. Nilikuwa naangalia hapa kama Afisa Mdhamini yupo hapa wa Pemba nilifanya kuuliza yupo hapa nikaona simuoni. Lakini naomba sana suala lile la Ziwani na la Ndagoni hususan suala lile la maji kama ile amri niliyoitoa mimi pale Mhe. Waziri kuweza kunisaidia kwamba mimi nakusudia wewe kazi na tunaisadia serikali kwa nia moja na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi basi wahakikishe suala lile la maji Skuli ya Ziwani wale walimu au kama walimu pamoja na wewe mwenyewe utajua mwenyewe vya kuyapata, lakini uhakikishe kwamba maji pale yamefika ili wanafunzi waondokane na dhiki ile.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame Ali wa Jimbo la Ziwani kwa mchango wako na nina imani kuwa waziri na watendani wamekuelewa, wamekusikia.

Waheshimiwa Wajumbe muda wetu kwa sasa umekwisha lakini jioni tutakuwa na mchangiaji wetu wa mwanzo Mhe. Simai Mohamed Said, Mhe. Bahati Khamis Kombo.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuakhirisha kikao hichi kuna tangazo hapa limeletwa kwamba Wajumbe wote wanaume wanatakiwa washiriki katika ufunguzi wa msikiti huko Chaani Banda Maji baada ya sala la Ijumaa ili kwenda kuunga mkono viongozi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe kikao nimeahirisha kwa sasa mpaka saa 11:00 jioni. Ahsanteni sana kwa utulivu wenu.

(Saa 5: 53 Mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 Jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na mpaka sasa nimemtaja Mhe. Simai Mohamed Said atakuwa mchangiaji wetu wa mwanzo, akifuatiwa na Mhe. Bahati Khamis Kombo, hao ndio waliokuwepo mpaka sasa hivi wachangiaji. Kwa hivyo, kama kuna wajumbe wengine ambao wanataka kuchangia nafasi ipo waweze kuchangia. Mhe. Simai Mohamed Said, atafuatiwa na Mhe. Bahati Khamis Kombo.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kukushukuru wewe kwa kuniona na kuweza kunipa nafasi na mimi ili kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu niweze kutoa mawazo yangu na fikra zangu ili niweze kuichangia ripoti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, juu ya taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya kamati ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Oktoba mwaka huu 2017.

Pia nitangulize shukrani zangu na pongezI kwa Mhe. Waziri ndugu yangu Mhe. Riziki Pembe. Kwa kweli maagizo yalikuwa ni mengi na wizara hii tunaifahamu kwamba ni katika wizara moja kubwa ambayo kila Mzanzibari au kila mwananchi inamgusa kwa njia moja au nyengine, au naweza kusema kwamba wizara hii ndio kitovu cha wananchi au cha serikali nzima juu ya mikakati yote ambayo tunaipanga ya Mkuza *vision 2020*, pamoja na mengineyo yote, tukiunganisha pia kwa kuzingatia *STGs* ambazo zimewekwa na Umoja wa Mataifa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimpongeze mzee wetu Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame pamoja na kamati yake yote kwa mambo mazuri ambayo wametuletea mbele yetu, ili tuweze kuyachangia.

Mhe. Mwenyekiti, nianze la kwanza kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein, kwa ziara nzuri aliyoifanya katika mikoa yote pamoja na Mkoa wetu wa Kusini, hasa katika kutilia mkazo katika suala zima la elimu na pia kuonesha umuhimu juu ya ziara yake katika mambo yote ambayo yanagusa wananchi, hasa suala zima la elimu na wapi anataka au ndoto yake inataka sisi Wazanzibari tufike.

Mhe. Mwenyekiti, moja nianze kwa kuanza kitu kimoja. Nimeangalia ripoti suala moja ningependa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atusaidie sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi *strategic* ya elimu ya Zanzibar. Naamini sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunahitaji kupata uelewa mkubwa sana, ili tuweze kwenda sambamba pamoja na serikali katika mpango mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, wengine tunaelewa juu ya ripoti ambazo zimetumwa Barazani hasa katika kuunganisha vyuo, lakini ingekuwa vizuri tungekuwa tunaanza kutoka skuli za maandalizi katikati mpaka juu, ili mpango wowote mkuu wa serikali kwenye suala zima la elimu tukenda sambamba sisi kama Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi, pamoja na serikali na wizara husika tukawa tuko kitu kimoja, kwa sababu hii wizara ina fikra nyingi na mambo mengi.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda kwenye agizo namba 4, nimeangalia masuala ya madawati, meza na viti juu ya mpango mkuu ambao serikali imejipanga. Kwa hivyo, ninanze kutoa pongeze kwamba tayari kuna mabadiliko makubwa katika wilaya zetu pamoja na maskuli yetu juu ya suala hili. Juhudi hiyo hiyo iliyoanza Mhe. Mwenyekiti, basi izidi kuendelea kwa kasi ili tuweze kutimiza jukumu letu na ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Pia niliangalia kwenye agizo namba 4 juu ya vitabu. Sasa ningependa Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie. Katika agizo namba 4 wanasema kwamba vitabu 192 vimekabidhiwa katika maskuli mengi, vitabu vya sayansi 192, halafu vitabu 335 vya sanaa na pia vitabu 6 vya somo la biashara. Nikiangalia kwa namba ya vitabu vilivyotajwa katika hii ripoti na katika mpango mzima ambapo kasi ambayo tunataka kwenda nayo naona ni kidogo sana. Kwa sababu ukiangalia kwenye hii inasema, wizara imegawa vitabu vya sayansi 192, vitabu vya sanaa 335 na vitabu vya somo la biashara 6 kwa skuli zenye kidato cha 5 na 6.

Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, ningeomba hivi vitabu ingewezekana natoa mawazo yangu hapa twende katika mpango ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wa sekondari hasa kidato cha tano na sita wanakuwa navyo. Sasa mimi nataka nitowe mawazo yangu katika njia moja, uzuri wa serikali yetu ukiangalia kutoka Mhe. Rais mpaka unakuja katika Shehia husika kila eneo kuna uongozi. Hapa nataka kuzungumzia Serikali zetu za Mikoa pamoja na Serikali za Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi bidii ikichukuliwa ya ziada kuwaunganisha nguvu za Serikali za Mikoa na Serikali za Wilaya kwa kutambua rasilimali walizokuwanazo za kiuchumi katika mikoa yao husika ili matatizo kama haya ya vitabu pamoja na mambo mengine waweze kuyapata kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano tuchukulie Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao umeshamiri sana katika biashara ya Sekta ya Utalii ambayo ni tegemeo la uchumi pia. Lakini ukiangalia mchango wa wawekezaji katika suala la elimu, kwa sababu wao pia ni mzizi ambao wanahitaji watu kuja kuwaajiri kutoka katika maeneo hayo hayo, basi wangeweza kusaidia sana katika masuala ya vitabu na kuboresha maskuli, endapo pangekuwa na pana mkakati maalum wa kusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi ninachokiona wizara husika iunganishe nguvu pamoja na Serikali za Mikoa, ambapo ikisimamiwa na wizara husika kwa vitabu ambavyo wanavyovitaka, kwa sababu wanafunzi wanatumia vitabu na serikali inakuwa inagawa vitabu. Lakini mimi naamini kwamba ipo njia unaweza kusimamia kwa kushirikiana pamoja na wakala mpiga chapa wetu wa serikali, tuka-*print* vitabu kwa wingi kabisa, tena sio vya sekondari tu, tukashuka mpaka vya *primary* na mpaka vya skuli za maandalizi, wale ambao wanahitajia vitabu vidogo vidogo vya kusoma vya kila siku, ili waweze kuvipata. Ikibidi tunaweza pia sisi Zanzibar tukaanza kufanya hata biashara ya kuuza vitabu kupeleka Tanzania Bara. Kwa sababu wakala wa mpiga chapa tunao, mashine tunazo, *designers* wapo. Kwa hivyo, tunachohitaji sasa ni kujipanga mkakati pale ambapo serikali inaweka nguvu zake, lakini yule ambaye atapenda yeye kusaidia au kuchangia katika mpango mkuu wa suala la vitabu, basi mimi naamini itawezekana sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Mwakilishi wa Jimbo langu la Tunguu nitakuwa niko tayari kabisa kusaidia kwa wanafunzi wangu wote wa sekondari wawe na vitabu vyote. Cha muhimu nipate zile *costing* aina za vitabu na baada ya hapo ni kulitekeleza tu basi, wala haina shida. Naamini kama tutaanza *pilot project* katika Mkoa wetu wa Kusini katika Jimbo la Tunguu, mimi vitabu vya sayansi nitahakikisha kwamba tunawasaidia wote kwa pamoja. Lakini leo kama mwakilishi tunasimamia mambo mengi sisi ya wananchi, kuna mambo kila siku ya afya, ya elimu. Lakini kama utaniletea *cost* ya vitabu ni hii nitafute njia ya kuunga mkono, kwa sababu serikali inatumia fedha nyingi sana katika sekta ya elimu, sekta ya afya na sekta ya maji, lakini haiwezi kufanya kila kitu na sisi lazima kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutafuta njia mbadala na ubunifu, ili kuweza kuiunga mkono wizara husika katika kutekeleza azma yake, na ndio sisi wanasiasa tunapenda tupate sifa na wananchi wetu watupende.

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri kwa wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu, niko tayari kushirikiana na wizara yake pamoja na serikali zetu za mikoa na wilaya, ili kulimaliza tatizo la vitabu vya sayansi na vyengine katika skuli zetu za sekondari katika Jimbo langu la Tunguu, ili kuunga mkono juhudi za serikali pamoja na ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini moja ambalo nimeliona katika agizo namba 4(f) suala la maktaba. Nimeona kuna mpango mkuu wa suala zima la maktaba za wilaya, ili kuhakikisha kwamba wilaya zote zitakuwa zina maktaba. Mimi nashauri Mhe. Mwenyekiti, hizi *library* zisiwe peke yake, kama tayari viwanja vimeshapatikana, vimeshapimwa na vimeshatayarishwa basi iwe ni *library* ambayo ni maktaba, lakini pia pawe pana *research center* kwa ajili ya wanafunzi wa sekondari wanapotaka kwenda kufanya *research* zao ndogo ndogo, sio *research* za watu ambao wanafanya kwenye shahada za *PhD*, hapana. Lakini pia wanafunzi sasa hivi wa sekondari wao wenyewe pia hufanya *research* zao ndogo ndogo ili kuongeza ujuzi wao na fani yao katika elimu ambayo wao malengo yao wanakusudia kufika baadae huko mbele.

Pia cha tatu, pawe pana *IT center* ya kutumia *Information Technology* mambo ya kompyuta, ziunganishwe zote katika eneo moja ili pachangamke, na maeneo haya pakiwa

tayari pameshapangiwa mpango mkuu na serikali, basi inakuwa ni rahisi sana kutafuta nguvu za nje pia ili kwenda nazo sambamba.

Kwa mfano, sasa hivi ukienda katika maskuli mengi wanataka kuweka kompyuta, sawa. Lakini pia utakuta katika kuunganisha hizi kompyuta kwenda kuziweka, suala la kupata *internet*, panakuwa pana ugumu, kwa sababu aidha itabidi watumie *internet* ya makampuni ya simu. Sasa mimi naamini tuanze kuweka katika maeneo hizi *center* za *IT* za wilaya pamoja na maktaba, ili wote hawa watakapokuwa na ujuzi wao hata kwa wale ambao watakuwa wamemaliza aidha hawajafanikiwa kwenda elimu ya sekondari basi wanaweza kujiendeleza kwa kutumia hizi *IT center* ambazo ni za wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini kwa nguvu ambazo, kama wizara itajipangia maalum katika maeneo haya basi inawezekana pia tukapata mafanikio makubwa kwa haraka, wanafunzi wetu wakafaidika sana na hata sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutapata wepesi sana na unafuu. Kwa sababu wakati mwengine unachangia kitu katika sehemu, baada ya muda panakuwa hapana usalama wake, pengine vijana huchukulia mambo mengine wakafanya wanayoyataka ambayo wanahisi wao ni sahihi. Mhe. Mwenyekiti, hizi sehemu tukiacha za *centres* zitakuwa ni endelevu na wengine watakaokuja baadae naamini wataweza kuziendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la *five percent* kwenye agizo namba 6, juu ya *five percent* ya *skill development levy* na suala la *vocation training*. Ukiangalia sambamba agizo namba 6 na namba 7, juu linavyozungumza suala zima la *STL* pamoja na Chuo cha Karume pia nataka nikigusie hapa. Najaribu kuvigusia kwa pamoja vitu viwili hivi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mwamini wa suala zima la kukikomboa Chuo cha Karume kukifanya kiwe kama kinavyohitajika. Nilikizungumzia wakati wa bajeti, mmezungumzia umuhimu wa ajira ambazo ziko nje tayari zinawasubiri, hasa katika kujiendeleza vijana wetu katika kuhakikisha kwamba chuo hiki kinapanda na kinakuwa zaidi. Mimi naamini nguvu na bidii iliyotumika na serikali hasa kwa upande wa Mhe. Rais, ambaye yeye pia ni *Chancellor* wa *State University* ya Zanzibar. Kwa hivyo, bidii na wizara husika iende katika hivi vyuo vyengine vidogo au hivi vyuo vyetu kama *Karume Institute of Science and Technology* au *KIST* ili haya masuala hasa katika *Marine Engineering, Mechanical Engineering, Electrical Engineering* ili katika ku- *create* hizi kazi tuweze kuzipata kwa ajili ya Wazanzibar, na hasa katika hizi mashine ambazo wanataka kutumia.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona katika eneo moja kuna juhudi zimechukuliwa juu ya chuo kimoja humo katika ripoti, sijui agizo namba ngapi lilikuwa. Wamejenga mahusiano na *Zanzibar Insurance Cooperation* au Shirika la Bima la Zanzibar, wapatiwe magari kwa ajili ya kufanya kazi zao za ufundi na za kujifunza. Sasa bidii kama hizi za kupata mashine kama hizi, mashine za *welding* za kisasa, ma- *switchboard, computerised* vitu vinavyotumika. Sasa leo Mhe. Mwenyekiti, ukienda pale Toyota unakuta gari zote sasa hivi Zanzibar zinahitaji kutumia *system* nyingi ambazo hasa za kutoka miaka ya 2010 kuendea juu, ukienda kuangalia unaambiwa inahitaji *computer box*, kikiharibika kitu inabidi uangalie *computer box*. Sasa vitu kama hivi vifaa tuhakikishe tunavipata na wanavitumia vijana wetu kujifunza kwa haraka. Mhe. Mwenyekiti, inawezekana badala

ya gari kutoka hapa Zanzibar kupelekwa Dar es Salaam kutengenezwa, basi tukaona gari inatoka Tanzania Bara zinakuja Zanzibar.

Mhe Mwenyekiti, ninaye rafiki yangu mmoja ana gari ya *range rover* ameitoa kutoka Zanzibar kaipeleka Dubai kuitengeneza, halafu ikarudishwa tena Zanzibar. Sasa kwa sababu *container* inaondoka Zanzibar tupu, akahisi bora alipie *container* akatengeneze gari yake Dabai halafu airudishe tena hapa. Sasa mimi naamini katika mambo kama haya tukiwa tuna vifaa vya kutosha vya kusimamia basi mabadiliko yatakuja mengi sana. Sasa katika *linkage* hizi za Chuo cha Karume, mimi ningefurahia walivyoongelea juu ya Chuo cha Karume wangekwenda kwa undani. Nilizungumza katika mawazo yangu wakati nachangia bajeti juu ya chuo hiki. Katika sehemu moja ambayo panahitajika pawe na nguvu na kuwa na *job center* ya vijana wetu ambao watakapotoka hapa kuwaunganisha na soko la ajira.

Mhe. Mwenyekiti, waziri wa utumishi nakumbuka mwaka jana nilipochangia na mwaka huu akaniahidi kwamba wao wataanzisha job *center* za wilaya, lakini hadi leo hizi *job centers* hazipo. Ukienda katika Wilaya yetu ya Kati yakuna eneo lililoanzishwa la *job centers.* Sasa mimi naamini katika vijana watakaotoka hapa, tuweke *job centers* katika vyuo kama hivi ili watambuwe ni soko lipi ambalo lipo tayari, na wale ambao wanahitaji. Kwa sababu utakuta katika mitandao ya wawekezaji, mitandao kwenye *face book* na maeneo mengine, mtu anauliza anataka mfanyakazi au fundi aina fulani, unakuta hakuna mtu anapata jibu. Lakini wapo vijana ambao ni *qualified* wako njiani lakini hawajui wapi wafike. Sasa tunawasomesha watu lakini hatuwaunganishi na soko la ajira lililokuwepo nje. Mimi naamini wizara japokuwa najua ajira ipo katika wizara nyengine, lakini kile kianzio waanze kuwalea wao, kwa sababu wanawalea wanawasomesha, wanapotoka nje kuingia mitaani, inabidi wanaingia kwenye njia tofauti. Tuwaelekeze katika zile hatua za awali ili waweze kufikia pale wanapopataka.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la ajira ambazo zilizokuwepo, usiangalie katika sekta ya utalii peke yale, tuwaangalie sisi wenyewe pia hawa vijana tunaowasomesha kwenda kutafuta ajira nje. Niliwahi kuchangia nikasema kwamba kuna ajira nyingi zinapatikana za mafundi na maeneo mengine, hasa katika nchi za Arabuni wanahitaji vijana. Siku hizi mabaharia vijana wetu Wazanzibari wengi wamechangamka, lakini miaka ya nyuma wanazidi. Sasa hivi kuna Chuo kinajengwa cha Ubaharia, naamini tukijipanga zaidi vijana wetu wengi wataingia, kwa sababu lengo la elimu mwisho ni kumfanya mtu aweze kujitegemea yeye mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa *issue* ya bodi za elimu za wilaya, zilikuwa zina umuhimu sana kufanyakazi pamoja na kamati za elimu za skuli, lakini hadi leo mbona pako kimya sana hizi bodi za elimu za wilaya ziko wapi na hawa ndio walikuwa washirikiane na kamati za skuli, ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kwa kasi katika suala zima la elimu.

Mhe. Mwenyekiti, naona tayari umeshaanza kuangalia saa yako. Kwa hivyo, mimi nimalizie tu kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi na nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa bidii zote. Mimi naamini hii ni katika wizara ambayo inayong'ara sasa hivi Mhe. Rais hajakosea. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutakuwa tuko nyuma yake

kumsaidia yeye, ili tuhakikishe kwamba tunafikia ile ndogo ya kuwasaidia vijana wetu katika suala zima la elimu kwa pamoja.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu, naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia kwa ripoti hii yote. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia machache kwa Laasiri hii. Kwanza kabisa nichukuwe fursa hii ya kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shein, kwa kuendelea kutuletea maendeleo na pia kututangazia juzi tu elimu bila malipo.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwa kumshukuru sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano mazuri waliyonayo, na pia mashirikiano mazuri waliyonayo wakiwa pamoja na kamati hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwenye ukurasa namba moja, katika pendekezo la kwanza. Hapa kamati inasema kwamba, huduma za lazima na miundombinu ziimarishwe katika skuli za maandalizi na msingi, upatikanaji wa huduma za lazima kama vile maji, vyoo na usalama wa skuli uhakikishwe kwa kushirikiana na mamlaka zinazotoa huduma hizo pamoja na upatikanaji wa fedha za bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo ya utekelezaji yanasema kwamba, katika kuimarisha huduma za lazima na miundombinu ya maji na vyoo katika skuli za maandalizi na msingi kwa mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na wafadhili *UNICEF*, *Milele Foundation, ZAWA, ADB, SOS na UMATI* walijenga jumla ya vyoo vipya 210 vikiwemo 38 vya watoto wenye mahitaji maalum. Aidha vyoo 270 vilifanyiwa ukarabati kati ya hivyo vyoo 236 kwa Unguja na vyoo 34 kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mweyekiti niwapongeze sana wafadhili wetu kwa jitihada kubwa ambazo wanazichukua kuisaidia jamii yote, lakini Mhe. Mwenyekiti niseme tu kwamba katika Jimbo langu Skuli ya Ngwachani bado ina tatizo la vyoo, namuomba Waziri mara hii na skuli hii nayo ikumbukwe tukizingatia sana katika jamii yetu tunatokewa na maradhi ya mripuko kama vile kipindu pindu na matumbo ya kuharisha damu. Hili ni tatizo kubwa kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba sana skuli hii ya Ngwachani Bondeni uweze kuikumbuka angalau nayo iweze kupata vyoo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika pendekezo la pili linasema kwamba kamati majengo ya skuli yafanyiwe ukarabati pamoja na kuweka uzio kwa maeneo yenye hali duni ya usalama. Mhe.Mwenyekiti, katika skuli yangu ya Dodo ni skuli ambayokuwa ina tatizo kubwa na skuli ile kwa kweli kama inawezekana basi Mhe. Waziri ingelivunjwa skuli ile na ikajengwa skuli nyengine kutokana natatizo walilokuwa nalo.

Mhe. Waziri ningeomba tu ukipata nafasi kama ni wewe au Naibu Waziri basi tufanye ziara uende ukaikague skuli ile na uione hali halisi jinsi ilivyo mule ndani basi ni tatizo na hatari hasa kwa wale wanafunzi wetu waliomo mle ndani.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika skuli ya Ukutini ina tatizo na tatizo lile nadhani hata Afisa Mdhamini wa Wizara ya Elimu Pemba analifahamu tatizo lile, kwa hiviyo ile skuli inahitaji kujengewa uzio. Kwa sababu pale limetokeza tatizo kubwa baina ya walimu kamati pamoja na vijana wetu kuunganisha na jamii yetu ya Ukutini, tatizo lile linasababishwa na uwanja wa mpira uliopo skuli. Lakini kama skuli ile itajengewa uzio basi naamini kwamba lile tatizo la kuwania ule uwanja baina ya vijana na walimu basi litaondoka kwa sababu wale vijana wataupata uwanja wao kucheza mpira bila ya matatizo ya ile skuli, ilifikia hadi kwamba kamati ya skuli basi walikatiwa vipande vyao, walimu walikatiwa vipande vyao, suala hili lilikuwa sio la kuridhisha katika jamii. Lakini yote haya sababu ya kukosekana kwa uzio ile skuli ipo pabaya na ubaya wenyewe lakini kwa sababu inakosa ulinzi, pale hapana mlinzi wao wenyewe walimu binafsi zamani walikuwa wakichanga pesa na kuwalipa walinzi lakini kwa kweli hivi sasa imekuwa ni vigumu kwa kiasi ambachokuwa wale walinzi wanataka pesa nyingi kuliko vile zamani walivyokubaliana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kwa upande wa skuli za maandalizi kwa kweli upande wa maandalizi katika jimbo langu zipo skuli nyingi lakini nazo pia zina matatizo ya walimu, ningependa sana kwamba skuli hizi wakati wale walimu ambao kuwa wameshapata mafunzo vizuri tu ya ualimu basi waweze kuajiriwa ili hili tatizo liweze kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti vile vile tukija katika skuli ya Wambaa ina wanafunzi wengi sana na skuli ile hivi sasa inasomewa na watoto kutoka Mgelema pamoja na Wambaa yenyewe hata na wa Chumbageni wote wanakwenda katika skuli iliyopo pale, limekuwa ni tatizo kwa wingi wa skuli na ukiangalia madarasa yaliyokuwepo pale ni kidogo. Pamoja na darasa moja ambalo limekarabatiwa lakini hali halisi haitosh, Mhe. Waziri nimuombe sana azipitie skuli hizi azingalie na pia azipatie ufumbuzi ili wale wanafunzi waweze kukaa madarasani vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache naunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi).*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia katika Wizara hii ya Elimu kwa utekelezaji wake wa maagizo ya kamati kwanza niwapongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara katika sehemu kubwa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati wamekwenda vizuri, hii inatupa mwelekeo mzuri na dhamira njema ya utekelezaji wa ilani ya CCM ndani ya Chama chetu cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi niende tu katika ukurasa namba 2 agizo namba 4 mfumo wa elimu wa maandalizi ya Msingi upitiwe na kuimarishwa zaidi katika kuhakikisha wanafunzi wanaotoka maandalizi kwenda msingi wana uwezo wa kusoma. Niipongeze Wizara imetoa maelezo mazuri katika utekelezaji lakini kuna eneo moja tu ambalo nilikuwa namuomba Mhe. Waziri na nalikariri maana majibu ni marefu mno, lakini nikariri pale ambapo nataka ufafanuzi wa ziada. Aidha Wizara ina mpango wa kujenga skuli mbili za maandalizi katika (Mlilile na Mbuyu Maji).

Mhe. Waziri maelezo haya yote kwa ujumla yalionesha kuwa program nzima ya Wizara ya Elimu katika ujenzi imeonesha kuwa kila shule zinajengwa kwa ufadhili na umeainishwa vizuri ndio maana nikasema utekelezaji mzuri, lakini eneo hili moja kuna kauli ya kuwa zitajengwa, lakini hatujui katika utekelezaji wake bajeti ipi. Sasa ilikuwa utwambie tu kwa sababu bajeti tuliyoipitisha skuli hizi hazikuonekana na hata katika wafadhili wanaofadhili hazikuonekana lakini katika utekelezaji umeweka, sasa ilikuwa tupate tu ufafanuzi wa ziada katika utaratibu wa sie tunaofuatilia utekelezaji wa ilani kwa umakini zaidi tuone bajeti ipi itakayojenga skuli hizi mbili. Lakini dhamira na ulivyoonesha tunakubali. Kwa hivyo tunataka kujua tu fedha hizi zinatoka wapi kwa sababu katika bajeti hatukutenga lakini pia Mhe. Mwenyekiti, katika wafadhili pia haikuonyeshwa lakini dhamira na utekelezaji wa Wizara umesema wazi kuwa watajenga.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika ukurasa Namba 4 kuna agizo pia la kamati ambalo walikuwa wanataka Wizara iwe na mashirikiano baina ya Wizara na Walimu, Wazee na Kamati mbali mbali ambazo zinasaidia mfumo wa wanafunzi katika elimu. Lakini hapa naomba nirudi nyuma kidogo katika kumbu kumbu za nyuma kidogo kipindi kama sikosei cha Mhe. Waziri wa Elimu Mwalimu Haroun Ali Suleiman, zilianzishwa bodi za elimu za kila Wilaya ambazo zilisaidia sana kutoa msukumo wa elimu kiwilaya. Lakini sasa zile bodi mimi sizioni maana naishi katika mazingira ya kulelewa katika Wilaya ya Kaskazini (B) lakini naishi kwa visa kidogo katika jimbo la Chumbuni Wilaya ya Mjini humu mote humu alau nawaza nikashitukizia alau uwepo wa zile bodi sasa bodi hizi sizioni utekelezaji wake.

Labda Mhe. Waziri atupe ufafanuzi kwa sababu huu ndio ukaribu wa ile jamii yenyewe katika usimamizi wa msukumo wa elimu bodi hizi bado zipo, na kama hazipo changamoto zake ni nini ili tuone ule msukumo wa elimu katika sura ya mashirikiano baina ya wazee na walimu unapatikana vizuri kupitia bodi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niende ukurasa namba 5 katika agizo la Kamati naomba nilisome kwa ufupi, linalohusu vitabu na vifaa vya maabara vipatikane kwa wakati. Mhe. Mwenyekiti, naomba hapa pia nishukuru sana majibu haya ya Wizara ya Elimu wakionesha takwimu nzuri za upatikanaji wa hivi vitabu lakini Wizara imegawa vitabu vya sayansi 192, vitabu vya sanaa 335 na vitabu vya somo la biashara. Sasa tulisikia kauli ambazo ni rasmin kabisa kuwa tuna uhaba wa vitabu vya uraia ambavyo vitabu vya uraia ni mali sana kwa utaratibu wangu mimi kwa sababu tunapata kujua au kuwajenga wale watoto wetu uzalendo wa nchi yao kwa sababu mambo mengi ndio yanazungumzwa hapo. Sasa kwenye eneo hili na utekelezaji wake na ni muhimu sana hatujaona kutajwa vitabu hivi vya uraia.

Sasa hemu Mhe. Waziri, katika kukuza ule uzalendo wa vijana wetu utakapokuja kwenye eneo hili tumefanikiwa kiasi gani maana utekelezaji basi uende katika maeneo mengine, maana hivi vitabu vya sanaa na biashara tunashukuru utekelezaji umekwenda vizuri lakini na hivi vinavyotujenga hisia na uzalendo wa nchi yetu viko katika hatua gani.

Lakini hapo hapo kuna agizo pia linalohusu maabara kwa ajili ya mitihani ya taifa kuna changamoto kubwa hapa pana changamoto mbili ambapo mara nyingi tunakuwa tunasikia hata wenyewe Wizara ya Elimu mnasema mna tatizo la walimu wa sayansi,

kwa hivyo tuna mpango pia tumeusikia hata katika tangazo la *tender* tulilolitoa juzi kuna mpango wa kujenga maabara nyingi kwa ajili ya sayansi, lakini kwa sasa tuone maana vifaa vyenyewe hivi mara zote tunapozitafuta tunavitafuta wakati wa mitihani ndio mara nyingi, sasa hebu tuone mkakati wa sasa hivi katika utekelezaji wake tumelenga kuvitafuta kwa sasa ili alau wakati wa mitihani viwepo au tunasubiri ule wakati mitihani, lakini tukishavipata changamoto ya pili inakuwa wale walimu.

Huu mkati wa kuwapata walimu angalau vifaa viwepo kwenye maabara zetu lakini na walimu wa sayansi wawepo vitu hivyo lazima viende sambamba, kwa hivyo Mhe. Waziri utekelezaji wa hili umesomeka lakini tunataka ufafanuzi wa ziada ili tuone hii kasi ya utatuzi wa suala la maabara kutoka vifaa na walimu wake kwa ujumla tunalipata na tunapata maelezo ya kina sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kunako ukurasa wa 7 kuna agizo la kamati la skuli za Sekondari na Ufundi ziimarishwa katika kupatiwa vifaa, lakini tumeona pesa zimetengwa hapa milioni 25 lakini Mhe. Waziri naomba ukubaliane na mie milioni 25 ni kidogo sana kwa vifaa vya ufundi, sasa tunajiuliza ndani ya Wizara ya Elimu nzima kwa vifaa vya ufundi katika maeneo ambayo mnayasimamia tutanunua kipi ambacho angalau iwe ni sehemu ya kukidhi lile eneo.

Lakini na hapa pia kutenga maana yake bado utekelezaji pia tunauona haujakamilika, labda Mhe. Waziri utwambie umetenga utanunua lini maana kutenga ni sehemu moja, lakini katika utekelezaji pia sehemu ya pili ni ivununue maana yake utwambie vifaa vimeshanunuliwa kwa sababu tuna miezi sita na pesa hizi ulitenga tokea bajeti ya Julai, tunamaliza pale tunakupa pesa nyengine pesa tayari imeshatengwa. Sasa tokea hapo tunapata jawabu pale imeshatengwa maana yake hata kamati inakuja mwezi wa Machi hii pesa ishatengwa sasa utekelezaji pia unaambiwa imetengwa si tatizo.

Lakini sasa hivi utupe tu *clarification* kuonekana baada ya hichi kikauli cha kutenga utatununulia lini maana kutenga umetenga muda mrefu lakini tuone maeneo hayo mawili hii pesa kwanza ni kidogo iliyotengwa, lakini pia umetenga lakini utwambie ni lini vifaa hivi vitanunuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika eneo hili kuna uhaba wa walimu wa ufundi kwa hivyo Mhe. Waziri pia katika utekelezaji mzuri na wananchi wetu ili wafahamu zaidi pia utwambie mna mkakati gani katika kutekeleza agizo hili la kamati katika kupata wale walimu wa ufundi ambao wana taaluma, ili vijana wetu wakiingia katika shule zile kama Mkokotoni na maeneo mengine ili tuone kasi ile inaendelea vizuri. Kwa sababu hata Mkokotoni tunaona wanafunzi wapo wanaoacha kusoma kule, wapo ambao wanaingia kwenye mawio wanasema walimu hawapo, kwa hivyo mambo haya yaende pamoja. Sasa naomba Mhe. Waziri agizo lipo nia safi ya utekelezaji ipo lakini tuone unatusaidia vipi katika kukabiliana na hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika ukurasa namba 9 wa Dakhalia, niwapongeze kamati kwa kuliona suala la dakhalia kwa vijana wetu hasa hawa wa kike, lakini Wizara imeweka mazingira mazuri ya dakhalia kwa sasa kwa watoto wa kike imeeleza vizuri

kwa ufupi na nasoma kwa sababu maagizo Mhe. Waziri kajitahidi kutufafanulia, lakini kuna maeneo tunataka uziada wake ili tupate faida kwa wananchi wetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tunaomba tu Waziri changamoto katika dakhalia bado zipo pamoja na jitihada za serikali na bado watoto wetu wanajipikia wenyewe hakuna utaratibu mzuri angalau na mfumo uliorahisisha wale vijana kupata *service* ya huduma zao kama za chakula. Lakini kama hawakujipikia wenyewe maana wakijipikia wenyewe athari za moto katika mabweni zinakuwa ni mtihani mkubwa lakini kama hawakujipikia ina maana watoke nje wakatafute. Sasa ule muda na dhamira ya kuwaweka katika eneo maalum kwa ajili ya kusoma ule muda unapotea na wanakuwa wanapata muda mdogo sasa hata wakipata huduma ile ya chakula. Sasa hebu tujue dhamira ya Serikali katika kuwarahisishia hili tutawasaidia vipi ili utekelezaji wa agizo hili uende sambamba na wanafunzi wapate unafuu zaidi wa kukabiliana na suala hili la chakula wanakuwepo dakhalia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka naomba niende katika agizo namba 14 ukurasa wa 11 Malengo na Miundombinu ya Vyuo na Vituo vya Amali yafanyiwe ukarabati. Pia hapa Wizara inasema imetenga kiasi cha Shs. 7,852,000/= kwanza nishukuru Serikali kwa kutenga pesa hizi Shs. 7,852,000/= ni fedha ambazo imetenga, lakini kauli yangu inajirejea kama ambavyo niliuliza kule kutenga tulitenga tokea Julai tulipopitisha bajeti ya mwaka 2017/2018. Kamati inapita agizo hili tayari mlishatenga tunataka kujua kutenga huku pesa tunafanikisha lini ili hili agizo liende sambamba kama dhamira ya kamati inavyotaka, maana bado tuna kauli ya kuwa tumetenga tumetenga lakini pia tunashukuru kwa azma hiyo ya kutenga lakini ufanikishaji ndio tunaotaka Mhe. Waziri ili tuende vizuri katika azma ya kutekeleza ilani ya CCM.

Mhe. Mwenyekiti, namba12 agizo la kamati Namba 17 Wanafunzi wapatiwe nyenzo za kufanyia mazoezi, kamati ilishauri Shirika la Bima la Zanzibar kusaidia kuwapatia vyuo vya amali kama Mkokotoni gari na vitu vyengine. Hapa uongozi wa mamlaka umepokea ushauri huo utafanya juhudi makusudi kuwasiliana na uongozi wa Bima kuona vipi mamlaka inaweza kufanya hivyo. Yaani hapa Mhe. Mwenyekiti, agizo hili lilitoka Machi, leo Mhe. Waziri na watendaji wa Wizara ya Elimu wanasema bado watawasiliana na hao viongozi wa Bima maana yake tuna miezi sita kuna kauli ya kuwa tunawasiliana, kuna changamoto hapa kati kati kuonekana Kamati ilishauri lakini agizo hili bado tutawasiliana ndani ya miezi sita mawasiliano haya hayapo hivi kweli agizo hili linaweza likatekelezeka, au labda ushauri wa kamati kabla haujaandikwa humu walikuwa watwambie tu huu ushauri umepokelewa lakini hautekelezeki.

Lakini kama unatekelezeka hatuoni sababu miezi sita Wizara ina watendaji wengi kuwa hatujafikia pahala tukaenda wenzetu wale tukakutana nao ili tukapata jibu linaloweza kutusaidia. Naamini wenzetu wana dhamira nzuri naomba sana viongozi wa Serikali yangu Wizara ya Elimu, Waziri pale najua mchapa kazi basi hili utusaidie sana ili tufike katika malengo ya utekelezaji wa ilani yetu.

Mhe. Mwenyekiti naomba nende katika agizo namba 18 ukurasa 13 Baraza la Mitihani la Zanzibar lipewe jukumu la kikamilifu la kusimamia mitihani ya Moko lakini pia maelezo ya wizara yametoka vizuri. Lakini mimi naomba tukubaliane na Mhe. Waziri kwenye

Baraza letu ambalo tunalitegemea yaani mpaka muda huu tunaoongea halina hata kalenda ya mitihani ya Moko na kuwa na Baraza la chombo kikubwa kile na hata hiyo kalenda hawajawahi kuimiliki mana yake ni dharura kubwa sana.

Sasa hebu Mhe. Waziri tunawashauri sana Baraza letu la mitihani liwe na kalenda yake maalum ambayo wenzetu wale wa NECTA wanafanya hivyo kwa nini na sisi Baraza letu lisifikie kulishauri likawa na kalenda yake maalum, sisi sote kama wazazi tukawa tunajua watoto wetu mwezi huu watakuwa na mtihani huu. Nikuombe tu Mhe. Waziri kwenye eneo hili utusaidie ili changamoto hii alau ya kuwa na kalenda tu ya Moko mitihani hii ya Moko hii tunaielewa, lakini Mhe. Mwenyekiti naomba nimalizie kwa kuwapongeza sana viongozi wa wizara ya elimu tumefanya kazi kubwa maagizo hayo ni sehemu tu ya utekelezaji wa yale mambo ambayo kamati imesema. Kamati hapa ripoti yao wamepongeza vizuri, wizara ya elimu wamefanya vizuri kwa hivyo hata mimi nasema napongeza vizuri naunga mkono hoja, pamoja na mchango wangu huo asilimia 110%. Mhe. Mwenyekiti, naomba kukushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Ahmada Yahya na baada ya Mhe. Ahmada Yahya nitampa nafasi Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na mwisho nitampa Mhe. Waziri afanye majumuisho ya yale yaliyochangiwa. Mhe. Ahmada.

Mhe. Ahmada Yahya: Ahsante sana, Mhe. Mwenyekiti nami kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia maelezo ya utekelezaji kwenye kamati hizi zinazohusika.

Kwanza awali ya wote namshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii, kuweza kusimama kwenye ukumbi huu nakushukuru na kunipa nafasi, lakini zaidi napenda kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuipa kipa umbele wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake yaliyopangiwa. Wizara hii ni wizara muhimu nawapongeza sana watendaji wake wote ni wachapa kazi kweli na hawalali kwa ajili ya kutupatia wataalamu wa kuongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Mimi niwapongeze kwamba wanakwenda katika hii sura inayosema Ikra kwanza someni kwanza, kwa hivyo wao wamekitita watu wetu, watoto wetu, wasome na watupe wataalamu. Katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti nitakwenda katika ukurasa namba 5.

Maagizo ya Kamati vitabu na vifaa vya maabara vipatikane kwa wakati badala ya wanafunzi kupatiwa vifaa hivyo miezi michache kabla ya kufanya mitihani. Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Waziri ni kweli hili ni tatizo wanafunzi wetu wanababaika sana siku za mitihani, na hasa muhula huu na mimi niseme tu nabahatika kuwaona namna wanapojichuja na kujipanga kufanya mitihani yao hasa maabara. Hapa mkazo uwepo na Wizara ya Elimu kuna usemi unasema "zima ni moto" wakati umewadiwa ndipo tayari watu wanaanza kufanya *direction* za kutafuta vifaa, tunaelewa duniani vifaa hivi ni ghali tena ni ghali mno, lakini uwepo mpango makhsusi wa kuweza wizara kuvipatia maskulini vifaa hivi mapema.

Mwenzetu wanajeshi kufanya manuva au *rehearsal*, wanafunzi wanatamani kabla ya mitihani wafanye mazoezi yao, ikiwadiwa siku za mitihani wanaanza kubabaika na ni hatari sana utaona vikundi, wanakusanya majani, konokono, nyoka na vyenginevyo kwa hiyo mimi nashauri wizara iwe na mpango maalum. Nimeona bajeti kwamba wametenga 139 milioni kununua vifaa napongeza lakini vinachelewa kufika maskulini.

Sasa hivi kuna gwaride huko la nje la mitihani ya taifa ilikuwa vifaa sasa hivi viwe vishafika na wanafunzi hawana wasiwasi, ili wanapoingia katika mitihani yao katika miezi michache ijayo wawe washawiva, kama askari mwamvuli, kwa hivyo nilikuwa nakariri mchango wa Ndugu yangu Miraji kutegwa ni suala mbali, lakini kutumia masuala mbali, na kufika katika pointi tatu, kutenga, kutumia, kufikisha subiri *implementation,* kwa hiyo mimi namshauri dada yangu Waziri na timu yake yote vifaa viwe vinafika mapema ndani maskuli. Kusudi wanafunzi waanze kujenga *confidence* ya kufanya mitihani yao kwa utulivu na amani ili tupate matokeo mazuri kwa wanafunzi wetu.

Mimi sina mchango mkubwa hapa, hapa ndipo penye maksi nyingi nime-*practice* kwamba wanafunzi wa sayansi wanakuwa makini sana katika *laboratory* kwa sababu pale panakuwa na pointi nyingi na nikiri tu kwamba wanasayansi tunawahitaji. Kwa hivyo mkazo uwekwe, wa vifaa viwe vinanunuliwa mapema zaidi wanafunzi wetu wapate kujilabu katika *loboratory* zao. Serikali imeandaa mpango mzuri wa Jamhuri ya Muungano na Zanzibar sasa hivi shule nyingi zina *loboratory* wenyewe nyingi tu, nimefanya *research* skuli za binafsi, skuli za serikali zina *loboratory* zao. Sisemi kama na hawa watu binasfi wasaidie lakini hizo ambazo za Serikali zijae na wanafunzi wapate wa kufanya shughuli hii kwa utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sina mchango mkubwa kwa namuunga mkono sana Simai Mohammed Said kwamba upande wa maktaba ndio msingi wa kujua mambo na dunia nzima, hizi maktaba za wilaya kama hazijajengwa basi kuwe na mpango mradi maalum wa kujenga maktaba za wilaya na kupatiwa vifaa ili hizi skuli za shamba shamba hizi ziwe hazina wasiwasi, vifaa vipo na wanajiandaa kwa mitihani na hao limbukeni hawatokuwa limbukeni kuja mjini kufata maktaba.

Kwa hayo machache mimi naipongeza sana wizara hii, na hata kitabu hichi kimeandaliwa kitaalamu sana tena, tena kitaalamu maana yake hata *type* imekwenda *level*. *K*wa hiyo nakupongeza sana sana na mimi sina wasiwasi naunga mkono sana hoja hii nawapongeza na waendelee kutoa elimu na taifa kulijitoa katika hali ya ujinga na tuwe katika hali ya watoto waliosoma na hata kuruka mbele. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana na kushukuru Mhe. Ahmada Yahya kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri, Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Waziri, Elimu na Mafunzo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa hii kuchangia machache na kutoa ufafanuni kwa masuala machache kabisa. Kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru sana sana Wajumbe wa Kamati ya Ustawi, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, tunashukuru kwamba wanaelewa kwamba na wao wanatekeleza Ilani ya Chama cha

Mapinduzi tunashukuru sana. Shukurani ya pili, pia tunawapa kwa sababu tunafanya kazi nao si ndani ya Baraza peke yake hata nje ya Baraza wanatushauri na tunafanya kazi kwa mashauri yao, tunawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulitolea ufafanuzi ni suala la Bodi za Elimu ni kwamba Bodi za Elimu zipo kisheria kwa mujibu wa sheria ya Elimu ya 1982, kuna Bodi ya Elimu, kuna Bodi za Elimu za Wilaya na wakati mwengine zitashuka mpaka chini Bodi za Elimu za skuli baadhi ya skuli. Kwa hivyo hizi zipo na zinafanya kazi zake na ripoti zake zinawasilishwa katika kikao vinachohusika. Mimi binafsi kama Naibu Waziri nimeshakutana baadhi ya viongozi wa bodi hizi, nimekutana na mwenyekiti wa bodi ya Wilaya ya kusini, wilaya ya Micheweni nimekutana nao kwa hivyo bodi hizi zipo na zinaendelea kufanya kazi.

Isipokuwa tunahitaji kujishajihisha zaidi ili kuweza kufanya kazi kwa uzuri zaidi na zaidi, nashukuru kwa wilaya ya kusini wameweza kuwahasisha kidogo wajumbe na wao wakahamasika wakashajiisha kamati za skuli kufanya kazi nzuri zaidi, kwa hivyo hii tunatoa pongezi maalum kwa wilaya ya kusini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti kuna suala jengine hili ambalo limeulizwa na Mhe. Mwakilishi wa Ziwani, nalo linahusu kukataliwa labda kwa mchango wake katika skuli hiyo tulimweleza Mhe. Mwakilishi kwamba sisi wizara ya elimu, tunafanya kazi kwa umakini mkubwa katika kupokea taarifa ambazo huwa tunaletewa. Tuna-*approach* tunaita *evidence case decision* kwamba tunatoa maamuzi baada ya kujiridhisha kwa ushahidi si kwamba mtu aseme neno tuchukue hatua na ndio maana tukamwambia kwamba suala lake linalichunguza, lakini bado akalazimisha tusema kwa hivyo tutasema baada ya kupata kufanya uchunguzi wa kina. Tulimwelekeza Afisa Mdhamini kufuatilia kwa makini suala hili katika skuli ya ziwani, akenda na timu yake maelezo tuliyopata Mhe. Mwenyekiti ambao nichukue fursa hii kuyasoma kwa uchache hatupendi hivyo lakini inabidi tuseme hivyo.

"Wanasema tulipata agizo kutoka Kamati ya Maendeleo kupitia Mwakilishi wa Jimbo, kuwa tufanye kikao tarehe 18/08/2017, tuliandaa kikao hicho bila ya kujua agenda rasmi ya kikao hicho, hivyo siku hiyo alifika Mwakilishi wa Ziwani saa 4.00 asubuhi lakini hawakuwa tayari kuzungumza kwa udhati, azma ya ujio wao huu na badala yake wakasema kuwa walileta msaada wa maji lakini kuna mjumbe mmoja wa kamati ya wazazi amezuia msaada huo jambo hili si sahihi. Pia akaacha agizo kwa Mwalimu Mkuu, kumuandikia barua ya kumfukuza mjumbe huyo jambo ambalo ni kinyume na utaratibu na kwamba hataki tena mjadili huo hili atalifikisha taarifa hii kwa Mhe. Waziri wa Elimu. Jambo la kusikitisha na kushangaza ni kuwa uongozi wa Skuli ulikuwa hauelewi chochote kuhusu msaada huo kwani si Mwakilishi au Diwani ambaye alifika hapo na kuzungumzia juu ya suala hili. Hivyo uongozi wa skuli unatoa tamko kwamba ulikuwa hauna taarifa ya suala hili ila kamati ya maji ya shehia ya ziwani ndio inaweza kutoa ufafanuzi zaidi. Kwa hivyo mwisho anasema tunaomba wale wote wanaoumwa na hili tukae pamoja tushirikiane ili tupate ufumbuzi wa tatizo hilo kwani umoja wetu ni silaha ya maendeleo yetu kwa ujumla kubwa zaidi ni kuwa tuelekeze imani zetu zote kwa wanafunzi ambao ni waathirika wakubwa wa kadhia hii".

Kwa hivyo ni taarifa ambayo nimeletewa kwa maandishi juu ya sakata hilo, kwa hivyo tumweleze kwamba Mwakilishi kwamba skuli ya ziwani iko tayari kupokea msaada wa mtu yoyote mwenye nia njema. Nataka nitahadharishe zaidi kwamba tunapotolewa taarifa lazima tuzichunguze, sisi kama viongozi wa wizara ya elimu tuliletewa taarifa za mwakilishi huyo, lakini tuliozichunguza kwa undani tukaona si kweli, kama tungelikurupuka tungekwisha mharibia jina lake kwa kweli kwa hivyo na yeye namshauri afanya utafiti wa kina kabla hajachukua uamuzi.

Suala la pili Mhe. ni suala la Skuli ya Ndagoni, suala hili tumelifuatilia kwa makini sana tukaunda Kamati kulichunguza zaidi ripoti imeshaletwa na tunaifanyia kazi zaidi kwa kuwa suala lenyewe uamuzi wake una *legal and potilical implication* baada ya kujiridhisha sisi tutataka ushauri zaidi kwa Mwanasheria Mkuu si suala la haraka haraka kwa hiyo aendelee kuvuta subra kwa sababu uongozi ni pamoja na subra ni pamoja na subra, hekima na ukomavu wa akili. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani, sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani wa kufafanua hoja zilizotolewa na wajumbe.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani: Mhe. Mwenyekiti napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufisha hadi muda huu tukiwa wazima na wenye afya njema lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa majumuisho kutokana na Ripoti ambayo niliiwasilisha ya Utekelezaji Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuwashukuru wajumbe wote ambao wamepata nafasi ya kuchagia ripoti yetu na nitapenda kuwataja Waheshimiwa ambao wamepata nafasi ya kuchangia.

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata - Jimbo la Kijito upele).

2. Mhe. Suleiman Makame Ali (Jimbo la Ziwani)

3. Mhe. Simai Mohammed Saidi (Mpakabasi - Jimbo la Tunguu)

4. Mhe. Bahati Khamis Kombo (Jimbo la Chambani)

5. Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza Jimbo la Chumbuni) pamoja na

6. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakili (Jimbo la Ikulu)

Mhe. Mwenyekiti, tunapenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wamechangia na hata wale waliokuwa hawakuchangia, naamini kwamba tayari wamekwisha kutuchangia katika siku nyingi lakini hata kwa mawazo wanatuchangia sana.

Mhe. Mwenyekiti, tuanze kwa kushukuru sana sana sana Kamati yako ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi na wewe pia ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, michago yote ambayo imetolewa hapa tumeipokea na tunaichukua kwa sababu mingi ni michango, michango ambayo ambayo yenye muelekeo ya kuboresha sekta yetu ya elimu ndani ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe, wamezizungumza zikiwemo Mhe. Ali Suleiman Ali alizungumza suala zima la mavazi kwa walimu wetu hasa wanawake, Mhe. Mwenyekiti, napenda sana kumhakikishia Mhe. Mwakilishi, pamoja na Waheshimiwa Wakilishi wote kwamba muongozo wa suala zima la mavazi tayari umetolewa na walimu wanafata hayo, lakini kama kuna walimu ambao wanakwenda kinyume na agizo hilo au muelekeo huo basi wizara yetu iko tayari katika kuzungumza na walimu hao lakini kuona kwamba wanafuata muelekeo ambao unatakiwa.

Suala la walimu kuvaa ndani ya skuli hiyo si sheria, nikabu walimu yeyote anaruhusiwa kuvaa akiwa njiani lakini anapofika skuli katika eneo la skuli lazima avue hiyo nikavu, na huo ndio utaratibu popote ulipo kwa sababu hata dini yetu haijalazimisha kwamba lazima tuwe tunavaa nikabu kwa hiyo mwalimu hakatazwi kuvaa nikabu katika mazingira yake ya njiani ama hata anapofika katika eneo la skuli, lakini akifika tu ndani ya eneo la skuli lazima nikabu hiyo aweze kuitoa.

Kwa Mhe. Mwakilishi ushauri wako tumeupokea vizuri na walimu wetu tutazungumza nao vizuri na hilo dokezo tayari tumelitoa lakini tutazidi kulifuatilia kwa namna ya walimu wetu ambavyo wanalifanyia kazi vile vile, tunapenda sana kuwaomba wawakilishi kwamba endapo kunatokezea lolote changa moto ndani ya Sekta ya Elimu, hasa katika maeneo ambayo tupo karibu tuambizane kwa haraka ili tuweze kuyafanyia kazi kwa haraka ambavyo baadhi ya wawakilishi wanafanya kazi kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, suala la vitabu limezungumzwa na Waheshimiwa wengi akiwemo Mhe. Simai Mohammed Said, Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mhe. Ahmada Yahya vitabu pamoja na vifaa vya sayansi.

Mhe. Mwenyekiti, vitabu ambavyo tumevizungumzia hapa, Mhe. Mwenyekiti kuna ambao wamechangia kwa maandishi ambao na nimeletewa hapa walasitoweza kusema ki hasa walichozungumza lakini napenda na wao waingie katika hansard Mhe. Zainab Abdalla Salum pamoja na Mhe. Khadija Omar Kibano wa Jimbo la Mtambwe nao pia wamechangia kwa njia ya maandishi. Tunashukuru sana kwa michango ambayo mmetupatia.

Mhe. Mwenyekiti, suala la vitabu ambavyo tumevitoa kwa madarasa ya *form five* na *form six* vile ni vitabu vya nyongeza ambavyo vitabu hivi tumevitoa kutokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi inayoongezeka siku hadi siku. Vitabu vile zaidi ni vitabu vya *reference* haina maana kama vile ni vitabu pekee ambavyo vinatolewa na Wizara. Vitabu

vipo lakini hivi ni katika nyongeza ya kuongezea ili wanafunzi wetu waweze kupata vitabu vingi, waweze kusomea kwa wepesi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Simai Mohammed Said yeye alisema kwamba yupo tayari kukaa na sisi na sisi tunamwambia na tunamuahidi kwamba tupo tayari kukaa na yeye katika kutatua matatizo yote ya kielimu ndani ya jimbo lake la Tunguu. Lakini kushirikiana na yeye katika kuona kwamba hivyo vitabu ambavyo ameeleza anavitafuta tutashirikiana na yeye na tuko tayari kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti, hata suala zima la kukaa na wawekezaji tayari tunafanya sana na serikali za Mikoa juu ya suala hili inalisimamia vizuri na Mikoa yetu yote wanazungumza na Wawekezaji na wale ambao wapo tayari kuchangia wanakuja ndani ya Wizara na wanapata fursa hiyo na wanachangia, muhimu tu kufuata masharti. Kwa sababu sio kila msaada unaokuja unaweza kuwa ni msaada inayosaidia. Kuna misaada mengine inakuja lakini kwa bahati mbaya inakuwa haisaidii sekta yetu. Hii imetokea mfano kuna vitabu vilikuja lakini ndani yake vina vipengele ambavyo vinapotosha maadili ya Kizanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo tunakubali tunapokea misaada lakini misaada hiyo ni lazima tuwe tunaiyelewa vizuri na tukubaliane nao serikali ili tuone kwamba maadili ya nchi yetu yanazingatiwa vizuri.

Vile vile suala la vitabu vya uraia Mhe. Mwakilishi wa jimbo la Chumbuni kwamba vitabu hivi vipo katika skuli za msingi kwa darasa la tano na sita na hakuna uhaba juu ya vitabu hivi vya uraia na vinatolewa ili kukuza uzalendo na muelekeo mzima kwa nchi yetu kwa vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, limezungumzwa vile vile suala la dakhalia. Dakhalia ambazo zimo kama nilivyozitaja katika ripoti yetu, ikiwemo dakhalia ya Fidelcasro, Uweleni, Mohamed Juma Pindua, Dakhalia ya Ufundi Kengeja na Karume, Dakhalia hizo zote zinapikwa ina maana kama wanafunzi kwenye Dahalia hizi hawapiki wao wenyewe na kuna Matron maalum na wapishi ambao wanashughulikia masuala ya mapishi na fedha za serikali ambazo zinatumika katika kuwahudumia wanafunzi hawa. Vile vile michango ya wazazi nayo inachangia katika kutoa huduma hizi kwa wanafunzi wetu.

Dahalia pekee ambayo haipikwi kwa muda huu ni Dakhalia ya Mazizini na hii ni kutokana kwamba Wizara inaendelea katika kuiratibu vizuri dakhalia hii ili katika mwaka 2018 iweze kuchukua wanafunzi wa kidatu cha tano wanawake kwa skuli za serikali zaidi, hasa kwa wale wanafunzi ambao wanaishi katika mazingira magumu. Kwa sasa Dakhalia hii inakaa wanafunzi ambao ni kutoka skuli tofauti hata za binafsi wanakwenda pale kwa ajili ya kukaa. Kwa hivyo hiyo ina maana kwamba hapapikwi kwa muda huu, lakini kuanzia mwakani huduma hizo kushirikiana na wazee zitaweza kupatikana vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala zima la ratiba ya mitihani, Mhe. Miraji Khamis Mussa ametoa mapendekezo yake tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Lakini hata hivyo mitihani

ya Moko ratiba yake hataweza kujitokeza kwani mitihani hiyo inaratibiwa na Baraza la Mitihani la Taifa na siyo Baraza la Mitihani la Zanzibar. Ina maana hii sisi hatuwezi kutoa mpaka wenzetu waweze kutuletea ratiba hizi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni suala la ununuzi wa vifaa vya ufundi kwa skuli mbili za Mikunguni pamoja na Skuli ya Kengeja. Tulizungumza kwamba milioni 25 zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa hivi. Tunaposema zimetengwa haina maana kwamba vifaa havinunuliwi, maana yake kama tayari zimetengwa na utaratibu wa kuagiza vifaa hivyo inakuwa tayari umeshafanyika. Ndio maana kwa sababu havijafika hatusemi kama tayari vipo, lakini vitakapofika basi hii sentensi nayo vile vile itaweza kubadilika. Sambamba na hili hata kwa vile vifaa vya sayansi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba vifaa vya sayansi ambayo tunaviagiza kwa ajili ya mitihani, vile vinakuwa ni vifaa maalum ambavyo vinatokana na *specification* kwa ajili ya ule mtihani husika. Kwa hivyo kama ni hivyo hatuwezi kununua vifaa hivi mapema kwa sababu hatujui *specification* itakuja vipi, wanzetu wanavyotuletea namna gani vitendo vitafanyika kwa ajili ya mitihani hii ya *practically* ndivyo ambavyo tunaweza kununua vifaa hivi na kuviagizia. Vifaa hivi vinakuwa vinawekwa katika skuli yaani vinawekwa mfano usiku wanafunzi wasione kwa sababu wanapoona maana tayari inakuwa ni mvujo wa ule mtihani. Kwa mnasaba huu vifaa hivyo haviwezi kuwekwa mapema na haviwezi kununuliwa mapema, vinanunuliwa pale ambapo *specification* zimeshatumwa. Lakini kwa vile vifaa vyengine ambavyo vinatumika kwa kila siku ni kwamba tunanunua na haina maana kwamba vinachelewa. Vipo na vinakuwa vinaongezewa kadri ya fedha inavyoruhusu, lakini tunashukuru kwamba vipo.

Waheshimiwa Wawakilishi si vibaya kwa yule ambaye ndani ya jimbo lake anahisi kuna tatizo na uwezo anao, tuchangie maendeleo ya elimu kwa pamoja kwa sababu elimu ni yetu sote. Tukishirikiana vizuri maendeleo ya elimu yataweza kupatikana vizuri, tukisema kila kitu tuiwachie Serikali kuna mambo mengine yatakuwa yanachelewa. Lakini kwa pamoja tuungane nguvu ili tuone kwamba maendeleo ya elimu yanaweza kufikiwa vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, matatizo ya maskuli mbali mbali ambayo yameelezwa na Mhe. Bahati wa Jimbo la Chambani. Mheshimiwa tumesikia kilio chako na sisi Wizara ama serikali kwa ujumla ni kwamba inapenda sana kutatua matatizo ya wananchi wake ndani ya maskuli na matatizo mengineyo. Naomba Mhe. Mwenyekiti, nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba tupo tayari kwenda na yeye pamoja katika hizi skuli zake kuziona hali ilivyo na kadri fedha itavyoruhusu katika bajeti yetu basi vile vile vyoo vya skuli zake vitapata kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Miraji Khamis Mussa alituuliza Skuli ya Mlilile na Mbuyu Maji fedha hizi zinatoka wapi kwa sababu katika bajeti hazikutokea. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa skuli hizi kwanza unakuja, tumshukuru sana Mhe. Mpendwa wetu Rais Dkt. Ali Mohammed Shein katika ziara yake ambayo aliifanya katika Mkoa wa Kaskazini Unguja wananchi wa maeneo haya walilalamika juu ya uhaba wa madarasa ama uhaba wa maskuli kutokana na umbali uliopo wa vile vijiji. Mhe. Rais alitoa ahadi kwamba serikali itajenga skuli hizi kuanzia kwa madarasa manne na ahadi kama

ambavyo Mhe. Rais ameiweka na Mhe. Rais ametoa agizo hili kwa Wizara na agizo la Mhe. Rais maana yake hiyo ni amri, kwa hivyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itajenga skuli hizi kwa kutumia fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika bajeti ya mwaka 2017/18.

Mhe. Mwenyekiti, tunawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi waone kwamba hizi zote ni juhudi za Mhe. Rais katika kuona kwamba Elimu bora kwanza kwa wote inafikiwa katika maeneo yote karibu hata maeneo yale ya mbali. Skuli hizi zitajengwa na fedha zetu na siyo za mfadhili wa aina yoyote kama ambavyo ilivyojengwa na Skuli ya Mgonjoni Wilaya ya Kaskazini (B) Unguja. Mhe. Mwenyekiti, nina imani kwamba Waheshimiwa watakuwa wametuelewa vizuri.

Mwisho kabisa suala la umeme katika Ripoti ya Kamati ambalo walilizungumza sana. Suala hili tayari Mawaziri wa Wizara mbili tumekaa pamoja pamoja na watendaji Wakuu wa ZECO na Karume na Kamati ya Utaalamu ya sehemu hizi mbili kwa pamoja inakaa katika kuona namna gani ya kulitatua tatizo hili. Tunaamini katika muda mfupi tu tatizo hili litamaliza na muwafaka utapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni hayo tu kwa leo ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wameomba wapatiwe ufafanuzi. Tuseme kwamba tunawashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa michango yenu na vile vile tunakushukuruni sana kwa mashirikiano ambayo mnaipatia Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Waheshimiwa nyote ndani ya majimbo yenu tunakushukuruni sana, mifuko mbali mbali ya majimbo ndani ya majimbo inafanya kazi. Tumekwenda Nungwi tumeona kwa Mhe. Ali Khamis Bakar na kwa Waheshimiwa wengine sitoweza kuwataja wote lakini hata jimbo la Mkoani Mfuko wa Mwakilishi nao umefanya kazi yake vizuri.

Tunaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tushirikiane kwa pamoja ili kuona kwamba "Elimu Bora Kwanza kwa Wote" inafikiwa vizuri, lakini jimbo la Chwaka vile vile Mhe. Mwakilishi anatoa sana maana yake zaidi ya mfuko wake wa jimbo mpaka fedha za mfukoni wanatoa. Anaezeka mabanda, anajenga nyumba za walimu, yote tunashirikiana na yeye vizuri. Kwa hivyo Waheshimiwa tunakushukuruni sana kwa mashirikiano ambayo mnatupatia. Lakini vile tunakushukuruni sana kwa kutueleza changamoto ambazo zinajitokeza ndani ya maeneo ambapo nyinyi kwa haraka haraka mnakuwa mnaziona.

Mhe. Mwenyekiti, tunakuombeni sana tuzidi kushirikiana ili kuona kwamba jahazi letu hili la elimu linakwenda vizuri. "Elimu Bora Kwanza" inawezekana lakini uzalendo wa nchi yetu ni muhimu sana. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni muhimu sana kuisimamia. Tushirikiane pamoja ili tuone tunafikia Ilani yetu ya Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 na tumuunge mkono Mhe. Rais wetu katika kuona kwamba maendeleo ndani ya nchi yetu yanafikiwa vizuri. Maendeleo hayaji bila ya kuwa na elimu bora, kwa hivyo tunaomba sana ili tuwe na wataalamu wazuri, tushirikiane vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru sana na nalishukuru Baraza lako Tukufu naomba kutoa hoja. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Waziri wa Wizara ya Elimu kwa majumuisho yako. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamaliza naomba niwahoji kama taarifa imepokelewa. Naona taarifa imepokelewa. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Nawashukuru sana. Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa *order paper* yetu ya leo shughuli zilizopangwa tumemaliza lakini kabla ya kuakhirisha naomba na mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wote waliochangia taarifa hii lakini pia nimpongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na watendaji wake wote waliomzunguka ndani ya Wizara yake. Shukurani za pekee niipongeze Kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri waliyoifanya ili kuhakikisha tunaleta maendeleo ya elimu ndani ya nchi yetu.

Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha naomba niwataarifu Wajumbe wote wa kuwa kesho tukijaaliwa kutakuwa na Semina ya kuhusu *Red Cross* na shughuli zake saa 3:00 asubuhi katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa utulivu wenu na michango yenu. Sasa naomba niakhirishe mpaka tarehe 9/10/2017 saa 3:00 asubuhi. Nawashukuru sana.

(Saa 12:02 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 9/10/2017 saa 3:00 za asubuhi)